NDIPO YESU AKAJA NA KUITA

. . .amini.

Hebu tusimame kwa muda mfupi tu sasa tunaposoma Neno la Bwana. Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, na kuanzia kifungu cha 18.

> *Na Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu, kadiri ya maili mbili hivi;*
>
> *Na watu wengi katika Wayahudi walikuwa wamekuja kwa Martha na Mariamu, ili kuwafariji kwa habari ya ndugu yao.*
>
> Basi Mariamu *mara alipo . . .ama Martha, aliposikia . . .kwamba Yesu anakuja, alikwenda kumlaki; na Mariamu alikuwa akikaa nyumbani.*
>
> *Basi Martha akamwambia Yesu, Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu . . .hangalikufa.*
>
> *Lakini hata sasa, najua ya kuwa yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.*
>
> *Yesu akamwambia, ndugu yako atafufuka.*
>
> *Martha akamwambia, Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.*
>
> *Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na . . . uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;*
>
> *. . .kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?*
>
> *Akamwambia, Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni.*
>
> *Naye alipokwisha kusema hayo, alikwenda zake; akamwita umbu lake Mariamu faraghani, akisema, Mwalimu yupo anakuita.*

2 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

3 Baba yetu wa Mbinguni, vile tulivyokusanyika hapa tena jioni ya leo kwa kusudi la kukutumikia Wewe, tukisoma Neno Lako, kuchukua fungu, na kuamini kwamba Wewe utatuletea na kutufunulia maana ya fungu hili. Tunaomba, Bwana, kwa ajili ya kila haja tuliyo nayo hapa usiku wa leo.

4 Huenda kukawa na baadhi wasiokujua. Jalia wakupate Wewe, usiku wa leo, kama Mwokozi wao na kulikubali hivyo. Jalia waweze, usiku wa leo, kwa jambo fulani linalofanywa, ama kusemwa, litakalomleta Kristo kweli halisi kwao. Kiasi

kwamba, hata maisha yao yote yatawekwa wakfu Kwake na kwa huduma Yake. Tunakushukuru kwa ajili ya mambo tuliyomwona akifanya na kwa ajili ya tumaini tulilo nalo la uhai kupita kivuli hiki tunachoishi sasa. Tukijua hili, kwamba ajapo tutanyakuliwa kumlaki hewani. Na pamoja na hili, Bwana, tunaomba ya kwamba utalitia tumaini hili, tumaini hili lililobarikiwa, katika moyo wa kila mtu, usiku wa leo. Wale ambao wamekuwa njiani kwa muda mrefu na kupitia mambo mengi magumu, jalia, usiku wa leo, imani yao iinuliwe. Wajalie, Bwana, kwamba watachukua mtazamo mpya, usiku wa leo, na kufanya upya nadhiri zao na kuanza upya tena.

5 Baba, tunawaombea wale ambao ni wagonjwa na wanaoteseka. Jalia huu uwe ndio usiku wa ukombozi wao. Wengi, Bwana, wameweka leso hapa jukwaani. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, wakati nikiweka mikono juu ya hizi ndani ya sanduku. Sasa, tunafundishwa, katika Biblia, kwamba, "Walichukua kutoka kwa mwili wa Mtakatifu Paulo leso na nguo, na roho chafu zikatoka ndani ya watu, na magonjwa yakaponywa." Sasa tunatambua kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Yesu. Na tunaomba, Bwana, kwamba Wewe utaponya kila mmoja ambaye leso hizi zinamwakilisha. Jalia wote waponywe kwa ajili ya Utukufu Wako.

Tumegee sasa Mkate wa Uzima, kutoka kwenye Neno, tunapongojea, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

6 Ni vema kurudi hapa tena usiku wa leo, na kumtumikia Bwana. Ni vema kuona orofa hii ya chini karibu imejaa, usiku wa leo, kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya kuhudhuria kwenu. Na kwa kuwa ni mara ya kwanza kuwa hapa, nafikiri ni vizuri sana.

7 Sasa, haijalishi ni wangapi tunaowazungumzia, tunazungumza jambo lile lile. Nimezungumza katika mikutano ya watatu tu ama wanne, halafu nimewazungumzia mia tano elfu kwa wakati mmoja. Mia mbili na hamsini elfu, wakati mwingine. Basi haijalishi ni nini, wale Kristo anaotuma kwangu, kusikiliza. Ninanena ninii . . . Nisingelibadilisha somo langu hata kidogo, kama hawa wangekuwa ni watu milioni moja wanaoketi hapa, usiku wa leo, vile vile tu. Maana, mimi ninapanda tu mbegu, Nayo haina budi kuanguka kwenye udongo mahali fulani. Na wakati mbegu hiyo ya mwisho itakapokuwa imeletwa ndani, hakutakuwa na la ziada. Tunajua huenda kukawa na ninii . . .

8 Tunashangaa ni kwa nini uamsho hauendelei hivi sasa, ni kwa nini hatuoni watu wakiwa na shauku. Sijui ni kwa nini. Lakini hebu tuwazie tu, vipi ikiwa hivi. Labda kuna mvulana mdogo humu ndani, usiku wa leo, ama msichana mdogo alizaliwa huko Seattle, Washington. Sasa, Kitabu hicho kinabeba jina lake. Alikuja kumkomboa ambaye jina lake liko

kwenye hicho Kitabu. Komboa maana yake ni "kurudisha kutoka mahali ilipoanguka kutoka." Na katika jamii ya wanadamu, yeye alianguka. Naye hawezi kulikubali sasa; angali ni mdogo sana. Kwa hiyo kanisa litaendelea kufanya uvivu, liendelee tu kucheza, litakuwa na mikutano, na kadhalika, mpaka huyo mtu wa mwisho atakapoingizwa ndani, ndipo Kitabu hicho kitafungwa, hakuna wengine wanaoongezewa. Basi imekwisha.

9 Mpaka, wakati huo utakapofika, hakuna mmoja wetu ajuaye. Lakini hebu tuendelee tu kufanya yote tuwezayo, kwa utukufu Wake, mpaka wakati huo utakapokwisha. Hatujui mtu huyo ni nani. Huenda ameingia tayari, tunangojea tu Kuja Kwake. Hatujui. Wala haitafunuliwa binadamu, wakati wa Kuja Kwake, kwa sababu hata Malaika wa Mbinguni hawajui kuwa itakuwa lini. Bali tunakutazamia tu wakati wowote, na kungojea, tukitazamia Kuja Kwake.

10 Sasa, inakubidi kuwa na imani katika jambo fulani. Haijalishi ni kitu gani, huna budi kuiweka imani yako mahali fulani. Imani yako, imani yako huenda ikawa katika ninii . . . katika kitabu cha kiada. Huenda ikawa katika kanuni yako ya imani. Kama hiyo ni ninii yako—kama hiyo ni imani yako, iko katika kanuni yako ya imani, basi hapo—hapo ndipo imani yako ilipo.

11 Tuseme, kwa mfano, dhe—dhehebu fulani, waseme, "Tuna kitabu cha kiada." Unaamini hicho. Vema, chochote nje ya hicho, huwezi kukiamini, unaona, kwa sababu hicho ndicho unachoamini, ni hicho kitabu cha kiada cha dhehebu hilo. Na huenda ikawa kwamba unaamini kitu fulani, unaweza kuwa na chaguo lako. Hicho ndicho wewe, sisi ni Wamarekani huru, kuwa hicho.

12 Bali, kwangu mimi, imani yangu iko katika Neno la Mungu, kile Mungu amesema kuwa ni Kweli. Mambo mengine yote kinyume na Hilo, kana kwamba sivyo. Mnaona? Sisemi kwamba sivyo, bali, kwangu mimi, kama ni kinyume na Hili, sivyo. Nasi tunapata leo hii kwamba watu wengi sana huiwekea msingi imani yao juu ya kitu fulani, na juu ya mfumo fulani, ama tukio fulani, au kitu fulani. Bali, kwangu mimi, haina budi kuwa ni Neno la Mungu, na Neno ambalo Yeye ameahidi kwa ajili ya siku hii.

13 Si torati. Torati ilikuwa kwa ajili ya Wayahudi, miaka iliyopita. Leo tuko katika milki za neema, na tuna—tunaishi juu ya sheria. Mtu ambaye—ambaye anaishi katika neema hana sheria. Hakuna sheria kwa neema.

14 Unawezaje kunihukumu kwa kuvuka taa ya kusimama hapa, ambapo jiji limenipa haki ya kuvuka taa yoyote ya kusimama nitakayo kuvuka? Mnaona? Usingeweza. Hakuna sheria ya kunihukumu.

15 Kwa hiyo, mradi tu niko ndani ya Kristo, niko huru na sheria. Mnaona? Niko juu ya sheria kwa sababu niko ndani ya neema Yake. Ameweka imani hiyo ndani yangu, kwamba sitatenda lolote lililo ovu, ama asingenipa neema hiyo. Hilo ndilo analokufanyia vile vile. Tuko katika neema Yake.

Sasa, somo langu, usiku wa leo.

16 Msisahau kesho usiku, sasa. Tutajaribu kukaa kwa muda mrefu zaidi kidogo tu. Ninataka nifike hapa mapema kidogo kesho usiku, kwa sababu ninataka . . . Kesho usiku ni namna ya usiku tunaotoa kwa ajili ya wokovu, kukazia tu mwito wa madhabahuni, kukazia wale watakao kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na usiku mmoja, ama siku moja, kabla sijaondoka, ningetaka kuzungumza juu ya ninii . . . somo la Damu, *Ile Ishara*, Damu inayopaswa kuwa juu ya mlango, na Bwana akipenda.

17 Sasa, usiku wa leo. Kila usiku, nimechelewa kila usiku. Nitajaribu kadiri ya uwezo wangu, usiku wa leo, kutoka kwa wakati ufaao. Natambua ya kwamba hatuna wakati mwingi sana uliosalia, nami najaribu kukomboa wakati ule tulio nao, kwa hiyo mvumiliane nami. Ninii . . . Nitaomba ya kwamba Mungu atachukua kila nafsi iliyoko hapa, iwezayo kuokolewa, naomba aiokoe. Sijui jinsi Yeye hulifanya. Na ni kazi yetu kutuma Neno, ama kulihubiri Neno. Na acha ninii . . . Hilo ni mbegu. Na wakati mbegu hiyo ikianza kukua, itazaa hasa kabisa kilicho ahadi.

18 Sasa kutoka katika Yohana Mtakatifu 11, usiku wa leo, tunachukua fungu hili: *Ndipo Yesu Akaja Na Kuita*. Yesu akaja.

19 Sasa tunapata msingi wa picha hii usiku wa leo. Ilikuwa ni Yesu, wakati alipokuwa ni ki—kijana tu, alikuja kuishi na familia fulani huko Bethania; na ilikuwa ni Mariamu na Martha na Lazaro. Nao walikuwa wameacha kanisa la—lao, ama kanuni yao ya imani ya Mafarisayo na Masadukayo, na walikuwa wamefanya urafiki na Yesu, na kumwalika nyumbani kwao. Naye Lazaro alikuwa rafiki Yake msi—msiri. Ndipo tunaambiwa, pia ya kwamba Lazaro vile vile alikuwa msikilizaji hodari wa Yohana Mbatizaji ambaye alikuwa akinena juu ya Masihi anayekuja. Hivyo basi wakati Yesu alipokuja jukwaani, na akaja Bethania, daima walimkaribisha katika nyumba hii.

20 Sasa, tunafundishwa ya kwamba Martha na Mariamu walifuma vitambaa vidogo vya ukutani kwa ajili ya hekalu, na kadhalika, ambapo Lazaro alikuwa akijifunza kuwa mwandishi, kuandika nyaraka za torati. Kwenye . . . Waliziandika juu ya ngozi wakati huo, kama vile ngozi ya mnyama, karatasi zilizotengenezwa kwa ngozi, kisha inakunjwa katika chuo kidogo na kutundikwa kwenye kishikizi kidogo. Naye Lazaro alikuwa stadi sana. Na angeweza kuandika magombo haya.

21 Naye Yesu alikuwa anakaa pamoja nao. Nao walikuwa wamemwangalia akifanya mambo mengi sana, walikuwa na

imani kubwa sana Naye, mpaka walikuwa wametoa tu maisha yao yote Kwake. Ingawa Yeye alikuwa . . .

22 Mnaona, Yesu, katika siku Zake, alidhihakiwa na kuchekwa zaidi, kuliko madhehebu ya chini kuliko yote duniani leo. Kusingeweza kuwa na chochote kilicho duni na kudharauliwa kuliko Yesu. Mnaona? Makanisa yalimchukia. Na hata hawakuwa na haja Naye, hata kidogo, kwa sababu sikuzote Yeye alikuwa akiwakemea, na kuwaita kila aina ya majina, na kuvunjilia mbali makusanyiko yao. Yeye aliupindua ulimwengu juu-chini kabisa, tuseme. Walikuwa wanajaribu kutafuta kasoro fulani, kumshitakia, nao wasingepata. Na hata hivyo alikuwa . . . Kwao, "Yeye alikuwa ni mwanaharamu. Alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Alikuwa ni mtu wa kipekee. Hakuwa na elimu ya ulimwenguni, tukinena, na hata hivyo alijiita Mwenyewe nabii. Na, loo, jamani, jinsi alivyokuwa jamaa wa kuchukiza!" Na kila mmoja wao alimkataa, kila mahali.

23 Haijabadilika sana. Mnaona? Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, "Ibilisi humchukua mtu wake bali si roho wake." Roho ya watu, iliyo ndani ya watu, imeishi hapo awali. Kama ilitupasa kuwa hapa kwa miezi kadhaa, ambapo tuna somo halisi katika Maandiko, ningetaka kuwathibitishia ya kwamba hakuna imani potovu juu ya uso wa dunia, leo hii, ila ile niwezayo kuwathibitishia kuwa ilianza katika Mwanzo, na kuwaonyesheni mwanzo wake. Ni mbegu, kama tu mzabibu ukikua, zote. Na unafikia moja kwa moja kwenye wakati wa kuchanua sasa, na kurudi tena kwenye—kwenye mbegu tena. Kwa hiyo mambo haya yote mnayoona yakitukia duniani, yalianza katika Mwanzo, kwa kuwa Mwanzo ndio sura ya mbegu ya Biblia, mwa—mwanzo.

24 Kwa hiyo mnaona, roho hizo, zilizokuwa juu ya watu hao huko nyuma katika siku hizo, zingali zinaishi juu ya watu leo. Mnaona? Shetani humchukua mtu, lakini roho huendelea kuishi.

25 Mungu humchukua mtu Wake, bali roho huendelea kuishi. Hiyo inamfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Alimchukua Kristo Yesu, lakini Roho, Roho Mtakatifu, alirudi, amekuwa juu ya watu Kanisani kote katika nyakati. Unaona? Kwa sababu, Mungu humchukua mtu Wake, bali si Roho Wake.

26 Shetani humchukua mtu wake, na unazipata roho zile zile. Angalia tabia zao.

27 Jitambulishe mwenyewe, usiku wa leo, katika hali yako ya sasa mahali unaposimama, na mtu fulani wa Biblia. Ungekuwa wapi kama ungaliishi wakati wa Nuhu? Ungekuwa wapi? Ungekuwa wapi katika siku za Bwana Yesu wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, katika mwili Wake? Ungetambulishwa na kundi gani, usiku wa leo? Liwazie tu. Unaona? Ungetambulishwa na kundi gani, wakati Paulo

alipokuwa akiwasahihisha huko nyuma katika Wakorintho kwa ajili ya mambo waliyokuwa wakitenda? Ungetambulishwa na kundi gani? Unaona? Tazama tu nyuma. Ni kioo cha kutazamia. Tunaweza kuona ambapo sisi, ninii . . . Chochote kile tulichokuwa, ndicho tulicho sasa, hicho ndicho tungalikuwa huko nyuma. Kwa sababu, roho iliyo ndani yetu sasa, ilitambulishwa huko nyuma, kwamba hiyo ndiyo roho ile ile iliyokuwa juu yao kule nyuma. Jamani!

28 Hiyo inapaswa kututikisa na kutufanya tutoke kwenye usingizi we—wetu tuliomo, vuguvugu. Lakini unajua Biblia inasema hatuna budi kuwa hivyo, ili kwamba aweze kutapika kitu chote kutoka kinywani Mwake. Je! aliahidi hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sote tunajua kwamba aliahidi hilo. Naye atalifanya. Kanisa lote litatapikwa kutoka kinywani Mwake.

Ndipo, kutoka kwenye kanisa huja Bibi-arusi. Huyo ni Mteule.

29 Sasa, Yesu alikuwa ameondoka nyumbani Mwake na alikuwa akiishi na Martha na Mariamu na Lazaro. Ndipo siku moja, unajua . . .

30 Alisema, katika Biblia, Yeye hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha la kufanya. Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile ambalo amwona Baba analitenda, hilo ndilo alitendalo Mwana vile vile." Na ukilinganisha Andiko hilo, tulikuwa na wakati wa kulichambua basi lingekuwa, lilionekana sawa, kwako. Unaendelea tu moja kwa moja . . . Linashikana kupitia Biblia nzima. Na kila kifungu katika Biblia kina hilo ndani yake.

31 Biblia iko katika mwendeleo. Kila Neno linashikana pamoja. Hakuna ukinzani ndani Yake. Yote inakimbia sawasawa. Ukipata ukinzani, umeupata *nje* ya Biblia, kwa sababu Biblia haijipingi. Iko katika mwendeleo, mwendeleo, kikamilifu. Tazama.

32 Sasa hili, Yesu, wakati . . . Alikuwa ndiye karama kuu kuliko zote Mungu alizowahi kuipa dunia, ulimwengu. "Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu," Yohana 3:16. Sasa, watu waliiamini.

33 Daima, karama za Mungu zinadharauliwa, na mienendo ya kisasa ya kidini. Tazama nyuma kwenye wakati wowote, katika siku za Eliya, katika siku za Musa, siku zozote kule unakotaka. Popote pale ilipo, inadharauliwa daima, sikuzote. Kamwe haibadiliki.

34 Halafu basi tunaona pale, pia, kwamba, katika siku hiyo, wakati Mungu akimtumia Yesu . . .

35 Sasa, kulikuwa na wakati ambapo mwanamke alitumia karama ya Mungu, kumpitia Yesu. Aligusa vazi Lake, na Yesu

akakubali kuwa hakujua ni nani aliyefanya hivyo. Sasa, siamini alikuwa tu ninii . . . Alifanya mzaha ama kuendelea. Ninaamini kila Neno ambalo alisema Yeye lilikuwa la maana, lilikuwa na maana. Na Yeye akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Hakujua. Ndipo akaangalia kote, katika wasikilizaji, mpaka akampata mwanamke aliyekuwa na imani hiyo, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu kulikuwa kumeponywa kwa sababu ya imani yake. Sasa, huyo alikuwa ni mwanamke huyo akitumia karama ya Mungu. Sasa, mnaona, mwanamke huyo mmoja akiitumia karama Yake, Yeye alidhoofika kutokana na hiyo.

36 Lakini angalia jambo hili hapa, wakati alipomfufua Lazaro kutoka katika wafu. Hakukuwa na chochote kilichosemwa kuhusu Yeye kudhoofika pale. Ni zaidi kiasi gani ilivyokuwa kumwita mtu, ambaye nafsi yake ilikuwa umbali wa safari ya siku nne, na uharibifu ulikuwa umeingia mwilini mwa mtu huyo! Pua yake, labda, katika siku nne, ilikuwa tayari imebonyea. Na Yeye hapo, akamwita kuwa hai tena, na akaishi, na akala, na akanywa, kama mtu yeyote mwingine. Hiyo ilikuwa kuu zaidi jinsi gani kuliko ilivyokuwa yule mwanamke kugusa vazi Lake! Lakini huyo alikuwa ni Mungu akitumia karama Yake. Mnaona?

37 Sasa, hiyo ndiyo tofauti hapa jukwaani. Sasa, kama ungefuatilia ninii—fuatilia ibada na uondoke, wakati mwingine, jinsi inavyosema mambo yatakayotukia, vema, miaka kabla, majuma kabla, miezi kabla, mahali pa kwenda, jambo la kufanya. Huyo ni Mungu akiitumia.

38 Hapa, ni wewe ukiitumia. Si mimi. Inapitia tu, maana ni karama tu ku—kujiachilia, kuiondoa kwenye gia ya binadamu, ili Mungu aweze kujitia gia Mwenyewe na Hiyo, na kusema mambo. Sasa, imani yako mwenyewe, hutambui hiyo, unafanya hilo, mwenyewe. Imani yako mwenyewe inafanya hilo.

39 Sasa, Mungu akitaka kufanya chochote, Yeye hukuinua tu, anasema, "Sasa, itakuwa, wewe nenda mahali fulani. Wakati ukiendesha gari barabarani, kutakuwa na jambo fulani litatukia *hapa*. Kutakuwa na mwanaume na ninii—amevaa suti ya hudhurungi. Ana mvi. Atakutana nawe pale chini. Wewe mwendee, maana mke wake ni mgonjwa sana. Mke yupo mahali hapa pengine. *Hivi* ndivyo atakavyoonekana. Basi nenda ukaweke mikono yako juu yake. Mwambie arudishe kitu hicho, alichochukua hapa miaka michache iliyopita, na kufanya jambo lingine, atubu, naye atakuwa sawa." Ndipo nitawaambia watu. Tunaenda. Huyu hapa mwanaume huyo pale. Kile hasa kinachotukia. Kuhusu mambo tofauti nchini.

40 Kumhusu huyu Marilyn Monroe wakati alipokufa, hawataamini ila kwamba msichana huyo alijiua. Lakini hakujiua. Alikufa kutokana na mshtuko wa moyo. Niliona, siku kadhaa kabla haijatendeka, na kuwaambia kuhusu jambo hilo. Bali wasingenisikiliza.

41 Wakati hao wapiganaji walipouana. Miezi sita kabla ya hilo kamwe... Huko juu New York, mmoja alimwua mwenzake. Niliwaona katika—katika vilabu vyao, wakibishana mmoja na mwenzake. Na kumwona mmoja akimwua mwenzake, miezi sita kabla haijatendeka.

42 Mambo haya yote ninii... ambayo Bwana huonyesha, hayo ni Yeye akitumia karama Yake. Hakuna ninii... Hudhoofiki, baada ya hayo. Lakini wakati... Hilo ndilo hunidhoofisha, ni wakati unapoitumia karama ya Mungu, kama Roho Mtakatifu. Mimi si karama Yake. Roho Mtakatifu ndiye karama Yake. Hiyo ni karama ya Mungu kwa Kanisa, ni Roho Mtakatifu, na mnamtumia. Naye hutumia tu popote unapoweza kujiondoa kwenye gia. Mnaona ninalomaanisha? Na kumwacha Roho Mtakatifu aanze kukutumia.

43 Sasa, katika jambo hili, Yesu alikuwa ameambiwa na Baba, aondoke nyumbani na kwenda mbali.

44 Mkitambua jinsi ilivyotukia, wao, baada ya Lazaro kuanza kuugua. Na hapana shaka, wengi wao walisema, "A-ha! Sasa hebu tuone alipo sasa yule mhubiri mtakatifu anayejifingirisha, anayeenda kuwaombea wagonjwa. Hayupo."

45 Kwa hiyo, Yeye aliondoka. Na wao, hatimaye, waliagiza aitwe. Wakati daktari alipomkatia tamaa, waliagiza kuwa Yeye aitwe aje. Na badala ya kuja, Yeye alizidi tu kwenda mbali. Wakaagiza tena aitwe. Na badala ya kuja, Yeye alizidi kwenda njia nyingine. Mnaona? Na kisha, ghafla, akasimama, akawaangalia wanafunzi; baada ya siku nyingi, ono lilitimiza kile Baba alikuwa amemwonyesha. Akasema, "Lazaro amelala."

Wanafunzi wakasema, "Vema, amefanya vizuri." Mnaona?

46 "Amelala," hajafa. Hakuna kitu kama mwaminio kufa. Mnaona? Na Yeye akawaambia katika lugha yao, "Amekufa, na kwa ajili yenu nafurahi kwamba sikuwako huko. Bali, naenda kumwamsha. Naenda kumwamsha."

47 Mnaona, alijua ilikuwa inaenda kutukia, sasa. Maana, kama hakujua, basi alisema jambo lisilo kweli wakati aliposema, "Sitendi lolote mpaka baba anionyeshe kwanza." Mnaona? Alijua hilo.

48 Halafu basi mwangalie kwenye kaburi, "Baba, nakushukuru Wewe, Wewe umenisikia tayari. Bali nasema hili kwa ajili ya wale wanaosimama karibu." Mnaona?

"Lazaro, njoo huku nje." Naye akatoka. Alitoka kaburini.

49 Sasa, wakati Yesu alipotoka nyumbani, mbona, kwamba kifo na shida zikaingia. Basi kumbuka tu, wakati Yeye anapoondoka nyumbani kwako, shida iko njiani. Sasa, Yeye hakuondolewa, hapa. Ama, Yeye aliondoka tu, kwa sababu Baba alikuwa amempeleka mbali. Matumaini yote yalikwisha. Sasa, ni maskini nyumba yenye huzuni jinsi gani! Wengi wetu, usiku wa leo,

wanajua jinsi ya kuihurumia nyumba hiyo, wakati kifo kimepiga nyumba yetu. Nawe hujui ni kitu gani mpaka inakubidi kuipitia wakati mmoja. Lakini, mnajua, wakati walikuwa ninii . . .

50 Kifo kilikuwa kimeipiga maskini nyumba hiyo. Walikuwa wameagiza aitwe. Jinsi nyumba hiyo ilivyokuwa na huzuni! Mtu yule waliyemtumainia, Mtu yule waliyempenda, Mtu yule waliyemwona akiwaponya wagonjwa, na kuwafanya vipofu kuona, na kutabiri, na kujua mawazo ya moyoni, na kuwaambia watu mambo yatakayotukia, kila wakati! Naye alitoshea Maandiko, kikamilifu, hasa kabisa, sana, mpaka watu wapenda Maandiko walimwamini. Mnaona? Na hao hapo baadhi ya rafiki zake waaminifu kuliko wote, Naye aliacha hilo litendeke. Mnaona? Aliacha hilo litendeke tu kusudi aweze kuona watakalofanya. Bila shaka, hilo ndilo lililokuwa niani mwa Baba kuhusu hilo. Matumaini yote yamekwisha. Mtu ambaye walimtumainia, iligeuka kuwa Yeye hakuwa kile walichomdhania kuwa, au ku—kuwa. Nao walikuwa wakidhikika. Lazaro, ndugu yao, alikuwa amekufa.

51 Wasingeweza kurudi kanisani, kwa sababu tayari walikuwa wamemkubali Yesu, “yule mlokole,” nao walikuwa wametengwa, na wana barua yao, kama ilivyokuwa, leo hii, kutoka kanisani mwao, hata wasingeweza kurudi. Nao waliachwa bila kanisa. Waliachwa bila rafiki, ilivyoonekana. Watu wa jiji hilo walikuwa wamewakana. Marafiki wao wema waliokuwa wakishirikiana nao kanisani, hawakushirikiana nao tena, kwa sababu walimkubali Yesu, “Huyu mlokole mwenye siasa kali.”

52 Kwa hiyo, basi, yule Mtu waliyemtumainia alikuwa amewakatalia kabisa na asingewafadhili. Nao wakaagiza aitwe kwa mara ya pili. Na Yeye bado aliwakatalia; na kumwacha mtu huyo kufa, akatiwa dawa, akawekwa kaburini, na kuzikwa. Sasa, wewe nena kuhusu wakati wa giza, huo ulikuwa ndio wakati wa giza kuliko zote nyumba hiyo ilipata kuona.

53 Ndipo Yesu akaja. Huyo ni Yeye, katika wakati huo wa giza. Yeye huiacha itukie, wakati mwingine. Wakati wa giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja. Uwepo Wake daima huleta matumaini mapya.

54 Huenda huu ukawa ndio wakati wenye giza kuliko zote kwa baadhi yenu. Huenda ikawa, daktari amekukatia tamaa, na kansa. Na mtu huyo amefanya yote awezayo kuyaokoa maisha yako, bali imepita maarifa ya—yake. Hana mengine ya kutumia. Amefanya yote awezayo, nawe utakufa. Huenda ikawa ndiyo saa yenye giza kuliko zote ulizowahi kuona. Lakini, kumbuka tu, ni wakati wa giza ambapo Yeye huja. Yeye huja. Basi, Yeye ajapo, huleta matumaini mapya. Huleta matumaini mapya Yeye ajapo. Uwepo Wake huleta matumaini.

55 Martha, alitoka nje. Daima alikuwa ameonyesha tabia yake, kwamba kwa hakika hakuonekana kuwa mtiifu kama Mariamu, kwa sababu Mariamu alikuwa akilisikiliza Neno, bali, Martha, wakati yeye alikuwa akimpikia chakula cha jioni, na kadhalika. Alidhihirisha kile alichokuwa pale pale.

56 Sababu, wakati Yesu aliporudi mjini, hapana shaka ila kwamba wengi wao walisema, "Sasa, baada ya huyu mvulana kufariki, na kuzikwa, sasa huyu mhubiri mtakatifu anayejifingirisha anarudi mjini kwa siri." Hapana shaka kwamba wakati Martha alipoanza kutoka, baadhi yao walisema, "Angalia, huyo hapo anaenda. Kama ingekuwa ni mimi, ningempa ukweli wa mambo. Ningemwambia wakati ningefika kule. Loo, hapana shaka atafanya hivyo. Tutaenda tumwone akifanya hivyo." Kama angefanya hivyo, hadithi hii isingesomeka jinsi ilivyo, usiku wa leo.

57 Sasa mwangalie. Huyu hapa anaenda. Huenda alipitia kwa nanii—nanii—mchungaji wa ninii lake—wa kanisa lake la awali. Naye akasema, "Sasa, hebu tuone kinachotukia sasa. Mnaona? Aliondoka kisiri. Wakati ule, wakati muhimu sana, ulipowadia, aliondoka kisiri."

58 Sasa, Martha, hapana shaka, alikuwa ni msomaji wa Biblia, la sivyo asingelimkubali Yesu, kuanzia. Asingelipokea juu ya saikolojia ya watu, ama juu ya msingi wa dini ya siku hiyo. Asingelipokea juu ya kanisa, kwa sababu kanisa lilimchukia. Nao wafuasi wa dini walimchukia. Na wote hao walimchukia. Kwa hiyo, hapana shaka alikuwa msomaji wa Maandiko, naye alikuwa amesoma katika Biblia.

59 Katika siku za Eliya, kulikuwa na mwanamke kwa ji-. . . kwa mwanamke Mshunami. Naye alikuwa tasa. Na alikuwa na imani katika mtu fulani, nabii, aliyekuwa wa siku hiyo, katika Eliya. Naye alikuwa amemjengea mahali padogo kando ya nyumba yake. Ama, yeye na mume wake walikuwa na nyumba nzuri. Walijenga mahali na kuweka ba—bakuli la maji mle ndani, na mahali kwa ajili yake kuoga na kujisafisha, na wakatengeneza tu mahali pazuri kwelikweli, panapopendeza. Ndipo alipopitia, yeye na Gehazi, mtumishi wake, naye akasema, "Tazama fadhili ambayo mwanamke huyu Mshunami ame—ametuonyesha." Kasema, "Nenda kamwulize kama nitazungumza na amiri jeshi ni—nimjuaye. Ninamjua vizuri sana. Ama, nizungumze na mfalme? Pia nimeitwa wakati mwingine kuzungumza naye na kushauriana naye." Kasema, "Sasa, sijui kama ninaweza kuzungumza na yeye nikienda mbele zake tena, ama nikiitwa kwa mmoja wa watu hawa?"

60 Kwa hiyo Gehazi alienda na akamwuliza. Naye akasema, "La." Akasema, "Ninaishi na watu wangu mwenyewe. Sina haja yoyote kuomba mambo kama hayo. Hiyo ilikuwa tu ni kutoka

moyoni mwangu, kwa sababu tu ninajua yeye ni mtu wa Mungu. Nami nataka kumfadhili. Hivyo tu." Akasema . . .

61 Vema, karudi, na Gehazi akasema, "Lakini mume wake ni mzee nao hawana watoto."

62 Kwa hiyo, hapana budi Eliya aliona ono. Kisha akasema, "Nenda, kamwambie, 'Panapo wakati wa uhai, yapata mwaka mmoja kuanzia sasa, atamkumbatia mtoto.'" Naye alimkumbatia. Alimzaa mvulana mdogo.

63 Mvulana huyo mdogo alikuwa na umri wa yapata miaka kumi na miwili. Alikuwa nje kondeni pamoja na babake, yapata saa tano mchana, kwa hiyo lazima ulikuwa ni ugonjwa unaotokana na jua kali. Alilia, "Kichwa changu! Kichwa changu!" Ndipo baba akamrudisha nyumbani, na—na kwa hiyo wakamlaza kwenye paja la mama. Na yapata adhuhuri, mvulana huyo mdogo akafariki, alikuwa mgonjwa sana; labda ugonjwa unaotokana na jua kali. Hakuna pumzi ndani yake. Alikuwa amekufa.

64 Kwa hiyo mama alimchukua akamlaza katika kitanda cha Eliya. Ni mahali pa jinsi gani pa kumlaza! Loo, jamani! Hakika kabisa. Alimlaza katika kitanda cha Eliya.

65 Naye akamwambia mtumishi, "Mtandike nyumbu sasa, na uende. Usisimame mpaka nikuambie, kwa sababu tunataka kumwendea mtu wa Mungu." Alijua, kama angeweza kumfikia mtu huyo, angejua ni kwa nini. Kama Mungu aliweza kumwambia mtoto huyo alikuwa akija, naye angembariki kwa baraka ya Mungu, kwamba ninii yake—kwamba tumbo lake la uzazi tasa lingemzaa mwana, hakika Mungu angeweza kumwambia mtu huyo ni kwa nini alimchukua. Akasema, "Usisimame mpaka nikuambie. Nenda kwa huyo mtu wa Mungu."

66 Sasa, wakati m—mpandaji alipofika karibu na mtu wa Mungu, yeye hakujua. Mungu hawaambii manabii wake mambo yote yatakayotukia. Hakujua la kufanya. Kwa hiyo alisema, "Huyu hapa yuaja yule Mshunami," alimwambia Gehazi. Kasema, "Na—naye ana huzuni, na Mungu amenificha hilo. Sijui analotaka."

67 Kwa hiyo, alipotokea. Ninalipenda hili. Alipofika karibu na Eliya, Eliya alipaza sauti, kasema, "Je! hujambo? Mumeo hajambo? Mtoto hajambo?"

68 Tazama, mume akitembea sakafuni, akipiga mayowe. Mnaona? Yeye hakuwa na imani ambayo mke alikuwa nayo. Na yeye, akipiga tu mayowe na kadhalika; majirani wote, wakiendelea. Naye mtoto, saa kadhaa kabla ya hapo, alikuwa amelala baridi, kitandani.

69 Angalia, wakati alipomfikia huyu mtu wa Mungu. Alisema, "Hatujambo." Amina. Napenda hilo. "Kila kitu ni shwari

sasa. Nipo katika uwepo wa mwakilishi Wake." Amina. Haya basi. "Hatujambo." Ndipo basi akasujudu miguuni pake na kuanza kumfunulia; si nabii kumwambia. Yeye ndiye aliyemwambia nabii.

70 Ndipo akamwambia Gehazi, "Jifunge viuno vyako, na uchukue fimbo hii uende ukaiweke juu ya mtoto huyo." Hakujua la kufanya.

71 Kwa hiyo . . . Nami nafikiri hapo ndipo Paulo, mtu mwingine wa Maandiko, asingewahi kabisa, kabisa kuchukua leso kutoka mwilini mwake, kama hakuwa na Maandiko ya kufanya hivyo. Eliya alijua kwamba, kila kitu alichogusa, kilibarikiwa; laiti angemfanya mwanamke huyo kuamini hilo! Basi nafikiri hilo ndilo Paulo alilofanya. Sasa, tunazitia leso mafuta. Sasa, hilo si la Kimaandiko, bali ni sawa. Hilo ni sawa kabisa. "Bali walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo," Biblia ilisema, "leso ama nguo." Tazama. Bali . . .

72 Ndipo Eliya, alisema, "Ichukue fimbo hii, nenda kaiweke juu ya huyo mtoto. Na mtu yeyote akizungumza nawe, usimjibu. Fululiza tu, uiweke fimbo juu ya mtoto."

73 Sasa, imani ya mwanamke huyo haikuwa katika fimbo. Ilikuwa katika nabii. Akasema, "Kama nanii—Bwana Mungu aishivyo, na nafsi yako haifi, sitakuacha." Naye akakaa moja kwa moja pale, aking'ang'ania, mpaka alipopata jibu la kile alichotaka kujua.

74 Vema, Eliya hakuwa na jibu, kwa hiyo kulikuwa na jambo moja tu la kufanya, kwenda pamoja naye. Kwa hiyo, alivifunga viuno vyake, na akaenda.

75 Alikutana na Gehazi akirudi. Kasema, "Je! ulitekeleza maagizo yangu?"

76 Akasema, "Naam. Niliiweka fimbo juu ya mtoto. Hakuna uhai wala chochote bado." Hiyo ilikuwa ni saa na saa nyingi mtoto akiwa amekufa.

77 Vema, Eliya akaingia. Hakujua la kufanya. Kwa hiyo, kumbukeni, alitembea huku na huku sakafuni, kwenda tu na kurudi, kwenda na kurudi, mpaka Roho akaja juu yake. Na wakati Roho alipokuja juu yake, aliulaza mwili wake mwenyewe juu ya mwili wa mtoto huyo, naye akapiga chafya mara saba na akafufuka, kwa sababu ya bidii na hiyo imani ya mama huyo.

78 Sasa, Martha, akijua kwamba huyu mwanamke Mshunami alikuwa na imani katika nabii huyu, akiwa ni mwakilishi wa Mungu duniani kwa ajili ya siku hiyo. Eliya alikuwa ndiye . . . alikuwa ni mwakilishi wa Mungu wa siku yake. Alijua kwamba alikuwa ameona ya kutosha kutoka kwa Yesu kwamba alikuwa ni mwakilishi wa Mungu wa siku hiyo. Haya basi. Mnaona? Yafanye maandiko kwenda sawa sawa.

79 Basi, alipopiga mbio kumwendea, na ilionekana kana kwamba alikuwa na haki kumkaripia, na kusema, "Kwa nini hukuja? Kwa nini hukuja? Tuliagiza uitwe. Tuliacha kanisa. Tulifanya *haya* yote." La. Hayo ni masimulizi yake ya 1964. Si wakati huo, mnaona. "Tulifanya *haya* yote. Tulifanya *lile*. Nilitoa *hili*. Nilitoa *lile*." Ulitoa nini? Mungu alimtoa Mwana kwa ajili yangu na wewe, tusiostahili.

80 Hapana budi alienda huko nje. Na alijua ya kwamba Mungu alikuwa amejidhihirisha Mwenyewe. Basi angalia anapokuja. Wanamfuata, kuona atakalosema. Sasa alienda huko nje, naye akaanguka mbele Yake, kwanza, kisha kasema, "Bwana." Hivyo ndivyo alivyokuwa. "Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Mnaona? "Ndugu yako asingalikufa." Ndipo yeye . . .

Akasema, "Ndugu yako atafufuka tena." Na Yeye . . .

81 "Ndiyo, Bwana. Atafufuka katika siku ya mwisho, katika ufufuo wa watu wote. Yeye alikuwa ni mvulana mwema. Atafufuka siku ya mwisho." Mnaona, waliamini katika ufufuo wa watu wote.

Yesu akasema, "Lakini Mimi ndimi huo ufufuo na Uzima."

82 Loo, jamani, baada ya kukataa mwito wake! Angewezaje Mtu, aliye Uzima wa kufufuka, kumtendea rafiki hivyo? Wakati mwingine Yeye anakujaribu, aone kile utakachofanya. Mnaona? Kuweka kitu hicho mbele yako, na kuona kile utakachofanya nacho. Huenda akafanya hivyo, usiku wa leo. Amekuwa akifanya hivyo, ili tu kuona utakachofanya kuhusu hilo.

83 Ndipo tunapata, kwamba hili lilipofanywa, alisema, "Ninaamini kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni." Hilo hasa ndilo alilokiri kuwa. "Na hata sasa, ingawa ndugu yangu amekufa, ingawa ametiwa dawa ya kuhifadhi maiti, ingawa amezikwa, ingawa ananuka kaburini, lakini hata sasa, chochote utakachomwomba Mungu, Mungu atakupa." Haya basi. Haya basi. Hilo ndilo jambo la kimsingi. Aliamini kile Yeye alichoomba. Kama Yeye alimwomba Mungu kwa ajili yake, Mungu angesikia maombi Yake. "Hata sasa, chochote utakachomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe."

84 Sasa ungeweza kuwa na aina hiyo ya imani, usiku wa leo, katika Neno la Mungu? Vema, Yesu ni Neno Lake. Unaweza kuwa na kiasi hicho cha imani katika Neno la Mungu? Wakati ni ninii tu—limetambulishwa moja kwa moja kwa ajili ya siku hii kama tu lilivyotambulishwa katika siku hiyo. Waweza kuamini hilo? "Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Mnaona?

85 Unasema, "Lakini daktari alinikataa, Ndugu Branham, kasema hakuna la ziada awezalo kufanya kwa ajili yangu."

86 "Bali hata sasa, Bwana!" Unasema, "Sijatembea kwa miaka. Lakini hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu

atakupa." Yeye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, akikungojea uombe. "Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu Wewe, Mungu atakupa."

87 Hivi Biblia haisemi, "Yeye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu"? Mkono wa kuume ni nini? Si mkono kama mwanadamu, wangu. Ni uweza, mkono wa kuume wa uweza. Yeye ni Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Mungu hapa sasa. Mkono wa kuume, aishiye daima Aliyepo, papa hapa. Wakati ukimhitaji Mungu, haikubidi kwenda Mbinguni. Yeye yupo papa hapa pamoja nawe. Mkono wa kuume wa uweza wa Ukuu Wake, ameketi hapa, tayari kufanya maombezi juu ya maungamo yako, akingojea kuitwa.

88 "Hata sasa, Bwana!" Ingawa daktari aliniambia nisingeweza kuishi ila juma jingine, "Hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa."

89 Si ajabu Yeye alisema, "Ndugu yako atafufuka tena." Akasema, "Mimi Ndimi huo ufufuo na Uzima. Aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na yeyote aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unayasadiki hayo?"

Akasema, "Ndiyo, Bwana, ninaamini." Jambo ndilo hilo.

90 Sasa, ukiwa na imani halisi, wakati meno hayo ya gurudumu yatakapokutana pamoja namna hiyo, gurudumu litageuka. Jambo fulani litatukia, maana kuna nguvu pande zote mbili. Nguvu, katika imani! Na nguvu . . . Gurudumu hilo dogo liligeuka kwa imani. Lile kubwa liligeuka kwa nguvu za Mungu. Wakati vitu hivyo vikianza kugeuka, jambo fulani halina budi kutukia.

91 Kufanya hiyo iwake hapo juu, inahitaji vipande viwili vya bidhaa, na dainamo, zikigeuka pamoja. Ni kama tu wewe. Itafanya nuru. Itafanya imani. Itafanya—itafanya nguvu. Itafanya uponyaji. Wakati mwaminio na Mungu wakigeuka pamoja, inazalisha nguvu za kufufuka Kwake. Wakati mwaminio akiweka Neno Lake ndani ya moyo wao na kuanza kuizalisha. Inaleta imani, maana ameahidi. Kila kitu kiko sawa sawa. Jambo la pekee unalopaswa kufanya ili kupata umeme ni kubonyeza swichi. Hayo tu ndiyo yakupasayo kufanya wakati Maandiko haya yanapaswa kutimia sasa. Bonyeza swichi. Usiogope.

92 Hiyo ndiyo shida ya watu. Nimesema mara kwa mara . . . Kidogo ni aibu kulisema. Ninapata makundi mawili ya watu ninaposafiri, wa kimsingi na Wapentekoste. Nje ya hao, sijui. Na wa kimsingi ni watu ambao kimahali wanajua wanaposimama, lakini hawana imani yoyote katika yale wanayofanya. Nao Wapentekoste ni watu ambao wana ninii . . . wanayo imani hiyo bali hawajijui ni akina nani.

93 Ni kama tu mtu aliye na fedha katika benki na hawezi kuandika hundi naye mwingine anaweza kuandika hundi na hana fedha katika benki. Laiti ungaliweza kuziweka pamoja.

Kama ukiwaamsha Wapentekoste, kwamba Roho Mtakatifu mnayedai kuwa naye, huyo ni Yeye akilitambulisha Jina Lake na Neno Lake. Basi tia sahihi ya jina lako katikati ya hundi na uisalimishe. Iangalie ikininii—iangalie ikitambuliwa na benki za Mbinguni.

94 "Ombeni Baba katika Jina Langu, lolote." Mnaona? Msiogope kuomba. Aliahidi atafanya. Mbona, hapo, hiyo... Haikupasi kuwa na wasiwasi juu yake. Yeye aliahidi.

95 Litazame sasa. Na yeye alikuwa sahihi, wakati alijua kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya. Alikuwa. Alikuwa. Alikuwa ni Kristo, pia. Mnaamini hilo? Yesu alisema alikuwa, alisema alikuwa ni mungu, maana Neno la Mungu lilimjia. Kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya, ni zaidi sana vipi alivyokuwa ndani ya Mwanawe! Na ikiwa Mungu, kwa sehemu hiyo ndogo, angeweza kumfufua mtoto aliyekufa, ni zaidi sana vipi, Mungu katika utimilifu Wake!

96 Vema, ni zaidi vipi sasa, Mungu akijitambulisha pamoja nasi na ndani yetu! Upatanisho umefanywa. Haukufanywa wakati ule. Walikuwa wangali chini ya upatanisho wa—wa kondoo wa kafara. Na sasa tuko chini ya upatanisho wa Damu ya Mungu; siyo damu ya Myahudi, siyo damu ya Mmataifa. Hakuwa myahudi wala mmataifa. Alikuwa Damu ya Mungu.

97 Damu hutoka kwa jinsia ya kiume. Kuku anaweza kutaga yai, lakini ikiwa hajawa na ndege wa kiume, halitaanguliwa. Halijarutubishwa. Kurutubishwa hutokana na himoglobini, hiyo ni damu iliyo katika jinsia ya kiume, daima. Mwanamke ni yai tu.

98 Na katika jambo hili, Yesu alikuwa ni Damu ya Mungu, seli ya Damu iliyoumbwa. Alikuwa si Myahudi wala Mmataifa. Alikuwa ni Mungu. Biblia ilisema, "Tunaokolewa na Damu ya Mungu," si ya Myahudi wala Mmataifa, Damu iliyoumbwa. Hapo ndipo, kama alikuwa ni Myahudi, imani yangu imekwisha. Kama alikuwa Mmataifa, imani yangu imekwisha. Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa ni Mungu asiyepatikana na mauti akidhihirishwa katika mwili, ambapo Yeye aliumba seli ya Damu na kufanya mwili Wake Mwenyewe. Amina. Hiyo hufanya pepo kutetemeka na kutoroka. Hiyo humweka mbioni. Wakati ukiona kitu halisi cha kweli. Msifu Bwana. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Mungu akidhihirishwa katika mwili. Yeye ndiye Damu ya Mungu. Hivyo basi, Uhai hutoka kwenye chembe hiyo. Na sasa kwa Damu hiyo...

99 Juu ya kafara ya kale, mwabuduo aliweka mkono wake juu ya kondoo dume, ndipo wakakata koo. Makuhani walichukua damu na kuiteketeza. Naye mwabuduo, akihisi uchungu wa kifo juu ya ko—kondoo dume, mikono yake yote imejaa damu kutoka kwa maskini kondoo dume, anayekufa, akifa, ama maskini kondoo, wakati akifa, bali alirudi na dhamiri ile ile alikuwa

nayo akija. Kwa sababu, wakati seli hiyo ya damu ilipovunjwa, ilikuwa ni damu ya mwingine, kondoo dume, unaona, na yai kutoka kwa jike. Na uhai uliokuwa katika hiyo usingeweza kurudi juu ya uhai wa mtu huyu, kwa sababu ulikuwa ni uhai wa mnyama. Uhai wa mnyama hauna nafsi, kwa hiyo hajui mema na mabaya. Kwa hiyo haungeweza kurudi.

100 Bali katika Hili, wakati kweli tukiweka mikono yetu juu ya Kafara yetu, Yesu, na kuhisi mioyoni mwetu kuwa tuna hatia, na kujua tutendayo. Damu ya Kafara hiyo, Uhai uliokuwa ndani ya Damu hiyo ulikuwa ni Mungu Mwenyewe, kwa hiyo anarudi juu yako, Roho Mtakatifu. Unafanyika mwana wa Mungu, basi, bila dhamiri yoyote ya dhambi. Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Hawezi kutenda dhambi. Mbegu ya Mungu imo ndani yake. Hawezi kutenda dhambi. Hana tamaa ya dhambi tena, hata kidogo. Kwa hiyo, mradi unatamani kutenda dhambi, una hatia kwake. Lakini wakati huna tamaa tena, ukifanya lolote baya, basi hulifanyi makusudi.

101 Waebrania 6 ilisema, "Tukitenda dhambi makusudi baada ya kuijua Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Kutenda dhambi makusudi. Kwa hiyo kama sikuzote unataka kutenda dhambi, makusudi, kuna kasoro fulani na ujuzi wako.

102 Sasa, wakati alipomsikia. Alikuwa moja kwa moja... Wakati aliposema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. MIMI NIKO." Loo! Ni hakikisho jinsi gani la Neno la ahadi, kwa kuwa Yeye alikuwa huyo MIMI NIKO aliyekuwa nyikani pamoja na Musa, huko nyuma katika kichaka kilichowaka moto! Hata wakati matumaini yote yalipotoweka, hata hivyo alikuwa ameridhika. Ikiwa tu angemfanya Yeye aombe, lingetukia. Sasa, jinsi tunavyohitaji imani kama hiyo leo!

103 Sasa, ilimbidi kuamini kwa ajili ya mambo yasiyowezekana, kwa mawazo ya kisasa, mwelekeo wa mawazo ya kisasa. Ilimbidi kuamini kwa ajili ya lisilowezekana. Bali mambo yasiyowezekana yanafanywa kuwa halisi wakati ukimwamini Mungu katika Neno Lake. Yasiyowezekana yanafanywa kuwa halisi wakati umemwamini Mungu katika Neno Lake.

104 Tazama, jinsi inavyopendeza, "Lakini hata sasa, Bwana, hata sasa," haijalishi jinsi ninii—hali ilivyo. "Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalitenda," katika saa hiyo yenye giza.

105 Hebu na tuwatazame watu wachache hapa, au hivyo, katika Biblia, kwa dakika moja tu, ili tu kuiona saa hiyo yenye giza kabla ya kuitisha mstari wa maombi.

106 Hebu tumwazie Ayubu. Alikuwa ndiye mtu mwenye haki kuliko wote duniani, ndipo Shetani akamjia. Kisha akaja kwa Mungu, kwanza, na kumshtaki Ayubu kwa kuwa tu kipenzi cha Mungu. Kasema, "Hakika, umemzungushia ua kote. Bomoa uzio huo. Nitamfanya akulaani usoni Pako."

Mungu akasema, “Huwezi.” Unaona?

107 Na sasa, Ayubu aliingia katika kila namna ya taabu. Kumbukeni, alipoteza mali yake yote. Alipoteza umaarufu wake wote.

108 Alikuwa ni mfalme, mwajua, huko Mashariki, na wafalme wote wadogo walikuwa wakija kusujudu mbele zake kwa sababu alikuwa ni mtu mwenye busara. Alikuwa ni nabii. Na kila mtu alitaka kumwona na kuzungumza naye, kwa kitambo kidogo tu. Muda mfupi tu wa wakati wake ungekuwa muhimu sana. Na jinsi alivyozoea kutembea barabarani, heshima moyoni mwake kwa Mungu, kwa kuwa Mungu alikuwa amemfanya nabii.

109 Nao watu wenye hekima wangekuja na kusema, “bwana, Ayubu, tunajua kwamba Mungu mkuu wa Mbinguni yu pamoja nawe. Tungetaka ushauri mdogo tu. Tumefanya jambo *fulani-fulani*. Tufanyeje?” Ndipo Mungu angemfunulia Ayubu. Nao wangeenda wafanye hilo hivyo, na hivyo ndivyo tu lingekuwa. Hilo ni sawa.

110 Bali, ghafla, watu wote walimgeuka. Naam. Kila mtu alimkataa. Ndipo tufani zikaja, zikawaua watoto wake na kuwaua mifugo wake wote. Kila kitu alichokuwa nacho kiliangamia. Basi kukaja baadhi ya wasiri wake kuliko wote, labda mashemasi wa kanisa lake, unaona, wakaja kumfariji. Nao walikuwa wakimshutumu. “Sasa, Ayubu, unajua, mtu aliyejaliwa na Mungu, kama wewe, na haya yote yamempata, lazima kuna kasoro fulani. Umefanya uovu fulani.”

111 Ayubu akasema, “Nimeridhika kwamba sina kasoro. Moyo wangu ni safi mbele za Mungu, na nimetoa sadaka yangu.” Amina.

112 Haya basi, basi simama juu yake. Ikiwa umetimiza matakwa ya Mungu, dumu papo hapo. Usisogee. Ibrahimu alikiita chochote kinyume na hiyo ahadi kana kwamba hakikuwepo. Hakusitasita katika ahadi kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu.

113 Ayubu alidumu nayo moja kwa moja. Baada ya kitambo, mke wake mwenyewe kwa namna fulani alimgeuka. Ayubu akatokewa na majipu, afya yake ikadorora. Alitoka akaketi kwenye lundo la majivu, na akajiparuza kwa kipande cha kigae au kitu kingine, kujiparuza. Hebu wazia tu jinsi mtu huyo alivyokuwa katika hali ya kusikitisha!

114 Ninakumbuka kuchukua hiyo wakati mmoja, kwenye maskani yangu, miaka iliyopita. Nami niliizungumzia kwa mwaka mzima, Kitabu cha Ayubu tu. Hiyo ndiyo njia. Tunaivunja tu, kulifunganisha tu Neno lote pamoja. Ndipo basi nikawa naye juu ya lundo hilo la majivu kwa yapata Jumapili tano mfululizo. Nami kamwe. . .Baada ya kitambo, maskini dada fulani akaniandikia barua. Akasema, “Ndugu Branham, ni lini utakapomtoa Ayubu kwenye lundo hilo la majivu?” Lakini

ni—nilikuwa nikijaribu kueleza jambo. Mnaona? Ni—nilikuwa nikifanya hivyo. Nilikuwa nikijaribu kuweka hili wazi, kwamba, ni kwa nini alikuwa pale.

115 Naye mke wake akatokea na kusema, "Ayubu, wewe ni mwenye mashaka. Mbona usimlaani Mungu na ufe mauti?"

116 Sasa angalia. Yeye hakumwita mwanamke mpumbavu. Alisema, "Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu." Kwa maneno mengine, "Wewe—wewe—wewe wanena kipumbavu." Akasema, "Bwana alitoa, naye Bwana ametwaa. Jina la Bwana libarikiwe."

117 Basi, alijua atakufa. Ndipo akasema, "Bwana . . . " Mlango wa 14 wa Ayubu, alisema, "Kuna matumaini katika mti, ukianguka chini." Alijua alikuwa ameninii . . . Ilishawishi watu. Maisha yake yalikuwa yenye manufaa. Mungu hatupi tu maisha yetu ili kuzurura tu huku, *hili*, *lile*. Alitupa, ili kumtumikia Yeye. Fanya jambo. Mwambie mtu mwingine. Huwezi kuongea? Imba kwa mluzi wimbo wa kanisa, ama kitu kingine. Toa ushawishi fulani, mahali fulani. Naye Ayubu alikuwa ni mtu mwenye manufaa.

118 Alisema, "Mti ukiingia chini kaburini; ha—harufu ya mvua, mizizi inatokeza tena. Ua likifa, maskini mbegu yake inakaa pale na kufunguka, shina hutokeza katika hiyo." Hakuna njia ya kuweza kupata uhai ndani yake. Lakini majira ya kuchipua yakiwadia, maskini ua hilo huchipuka tena. "Sasa, kuna matumaini, ua likifa, mti ukifa. Lakini mwanadamu," kasema, "hulala chini, yeye hutoa roho. Wanawe humletea heshima, wala yeye hajui." Ayubu ataka kujua. "Wakipanda mbegu ardhini, nayo huchipuka. Bali wanampanda mwanadamu ardhini, naye hachipuki." Sasa akasema, "Yote haya yanahusu nini?"

119 Naye asingeweza kuelewa hilo. "Jinsi mwanadamu, akiwa na utukufu zaidi kuliko ua; mwanadamu, utukufu zaidi kuliko mti, katika sura ya Mungu; na hata hivyo alimpanda ardhini, na hiyo—hiyo ilitosha. Wanawe walikuja kuomboleza, na yeye hajui. Laiti ungenificha kuzimuni, ukaniweka mahali pa siri hata ghadhabu Zako zitakapopita. Wewe huniandikia muda na mahali palipoamriwa; siwezi kupita."

120 Angalia sasa, wakati dhiki hii yote ilipokuja. Na marafiki zake wakampa kisogo, na kumshitaki kuwa ni mtenda dhambi kisiri. Mke alikuwa amemkana. Kila mtu alikuwa amemkana. Kasema, "Pumzi yake ilikuwa ya kigeni kwa mke wake." Na mambo yote yaliyompata! Na ilionekana kana kwamba Mungu alimkataa. Naye atakufa na kuingia chini ardhini.

121 Mungu alinena naye, kama vile tu kusema, "Ayubu, sasa jifunge viuno vyako. Naenda kuzungumza nawe." Ndipo basi wakati aliposema, "Unaona, mti haukutenda dhambi. U—ua halikutenda dhambi. Lilitumikia kusudi Langu. Kwa hiyo lilitiwa nguvu, moja na lingine, nalo halikutenda dhambi, kwa

hiyo linainuka tena. Lakini mwanadamu alitenda dhambi, kwa hiyo anakatiliwa mbali."

122 Kwa hiyo, basi, Ayubu akaanza kushangaa, na kisha akaingia katika dhiki kama tu Martha alivyoingia. Katika saa yenye giza, wakati, ushawishi wake wote, alikuwa ameuishi bure? Yeye angemzungumziaje Ayubu? Yeye ni nabii. Atamzungumziaje? Katika ono.

123 Basi akatazama juu, na ngurumo zikatoa sauti, radi zikamulika, na Yesu akaja. Ndipo akamwona katika siku za mwisho. Akasema, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya dunia hii. Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu ambaye nitamwona." Saa yenye giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja.

124 Sasa, hicho ndicho Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia. Ayubu, kiliandikwa kabla ya kuandikwa Mwanzo, wanadai hivyo.

125 Mwangalie sasa Musa, katika saa yake yenye giza. Alikwisha kujua. Mama yake alikuwa amemwambia jinsi Yehova alivyokuwa amemwinua, jinsi ambavyo yeye alikuwa anaenda kuwa mkombozi wa watu. Naye alikuwa amejaribu kuufanya kwa njia ya kijeshi, maana alikuwa ni mwanajeshi, aliyekuzwa na Farao, akawa ki—kiongozi. Alikuwa awe ndiye Farao anayefuata. Naye alienda kujaribu kuwakomboa kwa mkono wake mwenyewe.

Bali Mungu hakomboi namna hiyo. Mungu hukomboa kwa mkono Wake.

126 Kwa hiyo akawa mwerevu, akaelimika, akajifunza ninii yote. . . akapata Ph.D. yake, na LL.D. na ma LL yote na ma DD yaliyoambatana nayo, nadhani. Kwa hiyo aliwazia, "Kweli nimempata sasa. Mimi ni mbichi tu kutoka seminari." Kwa hiyo anakwenda pale nje, na akashindwa.

127 Ndipo Mungu akampeleka huko nje kwa miaka arobaini na kuondoa elimu hiyo yote kutoka kwake, unaona, miaka arobaini. Sasa yeye ni mzee, masharubu yakining'inia hata kufikia kiunoni mwake, fimbo mkononi mwake, matumaini yote ya kukomboa watu yametoweka. Maskini hao Waebrania huko chini, wakiteswa na hao manyapara, na kupigwa mgongoni, na—na wakanyaga matope katika matope hayo. Matumaini yote ya kukomboa yalikuwa yamekwisha. Ndipo basi siku moja, upande wa nyuma ya jangwa, Yesu akatokea, Nguzo ya Moto. Akasema, "MIMI NIKO."

Huyo Ndiye. Siku moja alikuwa akizungumza . . .

128 Akasema, "Mbona, Wewe unasema ati 'ulimwona Ibrahimu'? Mbona," akasema, "mbona, Wewe hujapitisha umri wa

miaka hamsini. Ndipo kasema...Tunafahamu wewe ni mwendawazimu. Wewe ni—Wewe una pepo."

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."

129 Kwa hiyo, Yesu alikuja, katika Nguzo ya Moto, kwenye saa yake yenye giza kuliko zote. Naye akashuka, wakati huo.

130 Mwajua, Yesu akikushika, hukufanya kutenda mambo yanayosikika kuwa ni wazimu, kwa ulimwengu. Ungeweza kuwazia mzee huyo akishuka kule kuuteka mji huo, au kuiteka nchi hiyo? Naye aliuteka, akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake, lakini yeye mwenyewe alikuwa katika mkono wa Mungu. Hiyo ndiyo iliyoleta tofauti.

131 Vema, hebu tuzungumzie mhusika mwingine kwa kitambo kidogo. Hebu tumzungumzie Yairo, katika Biblia, siku za Yesu. Yeye, yeye alikuwa ni jamaa mdogo mwema. Alikuwa ni mwa—mwaminio, mwaminio wa kisirisiri. Ningemwita kitu kama mwaminio mkwamia mpakani, kama wale wapelelezi waliovuka na kuonja mambo mazuri kisha wakarudi na kusema haiwezekani. Lakini Yairo aikuwa ni mwaminio wa kisirisiri. Alimwamini Bwana Yesu, maana alikuwa ni mtu mwema. Labda alisoma vyuo, na kuona mahali Yesu alitimiza matakwa haya yote, na Yeye alikuwa yule nabii aliyepaswa kuinuliwa, kulingana na Musa. Bali asingelikiri, kwa sababu, kwamba, yeyote aliyekiri kwamba walikuwa na Ye-...amekuwa huko nje na Yesu, vema, papo hapo walitengwa. Naye alikuwa ni kuhani.

132 Lakini, mwajua, Mungu anayo njia ya kushurutisha jambo, wakati mwingine, kukufanya utende hivyo. Kwa hiyo, mwajua, alikuwa na msichana mdogo, mtoto wake wa pekee. Naye akawa mgonjwa sana, nao wakamwita daktari. Naye daktari akafanya yote aliyoweza, naye mtoto huyo mdogo akaendelea kuwa mgonjwa zaidi na zaidi. Sasa daktari akamwita nje, kasema, "Yairo, nachukia kukuambia hili, Dk. ama Kasisi Yairo. Lakini wajua nini? Huyo mtoto yuaenda kufa. Anayo kama saa moja tu kuishi." Ninaweza kuwazia, wote katika jazba, na watu wamesimama karibu, wakilia. Ndipo wakamlaza katika kijitanda kidogo, kitu kama, sofa ndogo pale. Na ndipo Ye-...

133 Ninaweza kumwona maskini Yairo akizunguka ili kuichukua maskini kofia yake ya kikasisi, na kuivaa. Mke wake anasema, "Unaenda wapi?"

134 "Unajua, nadhani imenilazimu." Ndipo akatoka kupitia mlangoni. Ndipo kasema, "Wapi..." Mchungaji wake alikuwa amesimama pale, kasema, "Yairo, unaenda wapi?"

"A-ah, vema, niliwazia ningetembeatembea tu."

135 Mwajua, ni saa yake yenye giza kuliko zote. Huyu hapa akaja mtu fulani barabarani, kasema, "We, Yairo! Unamjua Yule aliye huko chini kwenye gati? Yesu Mnazareti, yule nabii, ndiyo kwanza afike." Ilikuwa ni saa yake yenye giza kuliko zote, ndipo

Yesu akaja moja kwa moja kwenye saa hiyo yenye giza. Ninaweza kumwona akiivuta kofia hiyo ndogo usoni mwake, na kuanza kwenda upesi awezavyo.

136 Akasema, "Bwana, njoo uweke mikono Yako juu ya mtoto wangu, naye atakuwa hai." Wakati akiwa njiani mwake akirudi, jambo la kwanza wajua, mtu mwingine alisema, "Usimsumbue. Yeye. . .Msichana amefariki tayari. Alifariki jana, naye amelazwa huko sasa." Loo, na yeye. . .Maskini moyo wake karibu upasuke.

137 Ninaweza kumwona Yesu akimwangalia, kasema, "Hivi sikukuambia, 'Usiogope nawe utaona utukufu wa Mungu'?" Ninawazia moyo wake ulirudi ukadunda sawasawa. Akapanda barabarani, akitazama kila msogeo. Aliingia nyumbani, wakasema, "Loo, amefariki."

Akasema, "Hajafa. Amelala."

138 "Vema," wakasema, "sasa sisi. . .Tumesikia Wewe ni mwendawazimu; sasa tunajua ndivyo ulivyo."

139 Akasema, "Tokeni, ninyi nyote msioamini. Siwezi kutenda lolote wakati ninyi msioamini mnaketi hapa." Akawatoa wote nje. Ndipo akamwendea mtoto huyo, kasema, "Amka, msichana," naye akaamka. Saa yenye giza kuliko zote, kifo kilikuwa kimeipiga nyumba hiyo, ndipo Yesu akaja.

140 Sasa tunatambua, wakati msichana wake mdogo alipokuwa mgonjwa, hakungojea, kama vile Nikodemo, kwa mahojiano ya faraghani usiku. Haja ilikuwa papo hapo. Ilimbidi kuingia kazini sasa hivi. Ni vivyo hivyo sasa hivi. Iwapo kuliwahi kuwa na wakati unapotaka kuponywa, sasa hivi ndiyo wakati. Usingoje wakati wowote mwingine. Huu ndio wakati wa kuingia kazini. Naam, bwana. Alidhikika, ndipo Yesu akaja na kumwita kutoka mautini.

141 Bartimayo kipofu, mhusika mmoja zaidi ambaye tungezungumzia, kwa dakika moja tu. Ningetaka kuwapeni hadithi ya maisha yake, jinsi yeye—yeye alikuwa, jinsi alivyopata riziki yake kwa hua wawili wadogo kucheza. Na kwa hiyo, katika siku hizo, walikuwa na mwana kondoo ambaye alimwongoza kipofu, jinsi tu walivyo na mbwa leo aongozaye kipofu.

142 Na kwa hiyo siku moja, hadithi inayosimuliwa kuhusu Bartimayo kipofu, kwamba, Yesu, kabla hajaja jukwaani, na kwamba alikuwa na msichana mdogo aliyekuwa mgonjwa. Naye aliambia. . .alienda na kulia na kumwomba Bwana, kasema, "Bwana, kama utaninii. . .kama Wewe ukinipa tu uhai huu wa msichana wangu mdogo! Sijawahi kumwona. Lakini kama utamfanya aishi, ninakuahidi, kesho, kwamba nitakupa Wewe hua wangu wawili." Hao ndio aliokuwa nao kutumbuiza watu. Ombaomba wengi, ilibidi awe na kitu kisicho cha kawaida. Kwa hiyo hua wawili wadogo wangepiga kichwangomba mmoja

juu ya mwenzake. Kwa hiyo akasema, vema, angeninii . . . Yeye alitoa, akatoa toleo hilo, kwa sababu mtoto huyo alipona.

143 Siku chache usiku baadaye, mkewe akawa mgonjwa. Naye akatapatapa kutafuta njia yake, kando ya nyumba, kasema, "Bwana, sina chochote kingine ila maskini mwana-kondoo wangu ambaye huniongoza." Akasema, "Kama utafanya apone," kasema, "Nita—nita—nitakupa Wewe mwana-kondoo huyu." Na kwa hiyo, kesho yake, mke wake akapona.

144 Kwa hiyo yeye huyu hapa, akishuka kwenda. Ndipo kasema, kasisi akasema, "Waenda wapi wewe, Bartimayo kipofu?"

145 Akasema, "Ninashuka kwenda kumtoa huyu mwana-kondoo." Kasema, "Mke wangu; Yehova alimponya mke wangu." Kisha kasema, "Naenda kumtoa mwana-kondoo huyu."

146 Kasema, "Huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo, Bartimayo." Kasema, "Mwana-kondoo huyo ndiye macho yako."

147 Akasema, "Lakini kama Bartimayo ataiheshimu ahadi yake kwa Mungu, Mungu atatoa mwana-kondoo kwa ajili ya jicho la Bartimayo."

148 Siku moja, alisikia makelele yakija kupitia mjini, baadhi yao wakipiga makelele, "Aise, Wewe nabii wa Galilaya, wananiambia ati Wewe huwafufua wafu." Huyo alikuwa ni kuhani. "Tunayo makaburi yaliyojaa wafu hapa juu. Njoo ukawafufue baadhi yao. Wananiambia ati Wewe huwafufua wafu. Hebu tukuone ukienda, kamfufue mmoja wao. Baadhi ya watu wema wamelala pale juu. Hebu tukuone Wewe ukiwafufua." Wengine wakasema, "Kama Wewe ni nabii, niambie nilichofanya jana."

149 Baadhi yao wakasema, "Utukufu kwa Mungu aliye juu! Mfungulieni njia Mfalme wa Israeli."

150 Kila namna ya ubishi, na mamia ya hao. Sasa, iwapo utaenda, ukipata kwenda Yeriko, na utambue alipokuwa ameketi, alikuwa karibu yadi mia mbili kutoka mahali walipotokea langoni. Sasa, hapana shaka, watu wakivurugika juu yake. Naye maskini mzee huyo ameketi pale kwenye upepo, akitetemeka, amejizungushia matambara. Na hakuna mwana-kondoo wa kumwongoza, wala hakuna—wala hakuna hua. Na labda alikuwa hana makaa kwa ajili ya majira ya baridi kali, na ni . . . huenda ilikuwa ni Oktoba, na kulikuwa baridi. Naye hapo ameketi, katika hali hiyo. Na yeye . . . Mama fulani mwema hapana shaka alimwambia, wakati . . .

151 Akasema, "Nani? Kelele hizo zote ni za nini?" Unajua, kuna kitu kisicho cha kawaida. Alipo Yesu, daima kuna kelele nyingi. Naam. Kweli. Akasema, "Kelele hizi zote ni za nini?" Vema, wakasema . . .

152 Huyu mama mwema, lazima alikuwa mfuasi wa Yesu. Akasema, "Unajua, ni Yesu wa Nazareti."

"Vema, Yesu wa Nazareti ni nani?"

153 "Vema, unajua, Maandiko yanasema kwamba Bwana Mungu atamwinua nabii."

"Loo, naam! Unamaanisha Mwana wa Daudi? Je! Yuko duniani?"

"Nimemwona akifanya hasa. Yeye ni neno. Hiyo ni hakika."

154 Akapaza sauti, "Ewe, Yesu, kuwa. . .Ewe, Yesu, Mwana wa Daudi, nirehemu!" Sasa, alijua. Alikuwa amepita tayari. Alijua kilio chake cha kimwili hakingeweza kusikika. Lakini alijua, kama Yeye alikuwa ni Neno, na Yeye alikuwa ni Masihi, ilibidi awe ni nabii, maana Masihi alikuwa ni nabii. Naye alijua kwamba angeweza. . .imani yake kwa Mungu. Hapana shaka kwamba alipaza sauti, "Yehova, nirehemu! Nirehemu! Sasa hebu niweze kumsimamisha." Naye akalia, "Ewe Mwana wa Daudi, nirehemu!" Labda, makelele yote, asingeweza kusikia. Lakini imani yake ilimsimamisha. Yesu alisema hivyo.

155 "Ndipo Yesu akasimama kimya." Ninataka kuhubiri juu ya hilo, labda, wakati mmoja, siku. "Ndipo Yesu akasimama kimya."

156 Ndipo akasimama kimya. Akaangalia kote. Ndipo akasema, "Imani yako imekufanya mzima." Kwenye saa yenye giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja.

157 Asubuhi kabla tu ya hiyo, kulikuwa na ninii. . .wakati Yeye. . .asubuhi kabla tu ya Yeye kuingia, akitokea langoni alasiri hiyo. Alikuwa amekuja mjini, kulikuwa na mtu pale jina lake Zakayo. Naye alikuwa ni mfanyi biashara wa mjini. Naye mke wake, Rebeka, alikuwa ni mwa—mwanamke mwema, mwaminio wa Bwana Yesu.

158 Bali mwenyewe, hakuamini, maana rabi alikuwa amemwambia, "Hakuna manabii. Hatujawa na manabii. Hilo ni lundo la upuuzi. Usiamini kitu kama hicho. Wewe ni mtu mwungwana sana; biashara yako hapa. Mbona, kamwe usifanye hivyo. Angalia cheo chako kanisani."

159 Na kwa hiyo alikuwa amemwambia Rebeka, kasema, "Lo, huo ni upuuzi. Hakuna kitu kama nabii."

160 Lakini, unajua, Rebeka alikuwa ameomba; mpaka maskini moyo wake karibu upasuke. Alitaka kujionea mwenyewe. Kwa hiyo alijua Yeye alikuwa awe mjini siku hiyo. Kwa hiyo unajua alichofanya? Alikuwa mdogo wa kimo, kwa hiyo asingeweza kuninii—kumwona wakati akipita, kwa sababu ya umati. Kwa hiyo akasema, "Nitaona ikiwa Yeye ni nabii au la. Nikimwangalia usoni, nitajua kama Yeye anaonekana kuwa tofauti na mtu yeyote mwingine." Kwa hiyo akapanda juu mtini, na kuvuta majani yote kujifunikia, na kadhalika, na kuketi pale. Kisha kasema, "Sasa, wajua, wakati akipita, nitamwona."

161 Kwa hiyo alipokuja kwenye kona, akitembea *hivi*, akitembea kushuka barabarani, akafika moja kwa moja chini ya mti. Ndipo akasimama, akaangalia juu, akasema, "Zakayo, shuka chini. Naenda nawe nyumbani." Loo, wakati wake wenye giza kuliko zote. Hivi Yeye alikuwa ni nabii au Yeye hakuwa ni nabii? Kwenye saa yenye giza kuliko zote, Yesu akaja. Alijua kuwa alikuwa ni nani. "Zakayo, shuka chini."

162 Zakayo akasema, "Kama nimetenda kosa lolote, nitalipa. Nitafanya chochote." Alishawishika. Yesu alikuja.

163 Mwanamke aliyetokwa damu alikuwa ameenda, Biblia ilisema, "Alitumia fedha zake zote kwa madaktari. Hakuna hata mmoja aliyeweza kumsaidia." Hapana shaka, madaktari walijaribu sana, lakini walishindwa. Wasingeweza kumsaidia. Alikuwa ametokwa damu kwa miaka na miaka, labda tangu wakati wa kukoma hedhi. Naye alikuwa ni mwanamke mzee sasa, na kulizidi tu kuendelea. Asingeweza kukomesha. Loo, alikuwa . . . Alikuwa katika kudhikika. Kwa sababu, bila shaka, asubuhi hiyo wakati ninii ndogo—mashua ndogo ilipotia nanga kwenye miti mirefu myembamba pale chini, mtu fulani . . . Yeye aliishi juu kwenye kilima, juu. Labda mume wake alikuwa ameuza farasi, na—na shamba aliliweka rehani, na kila kitu, akijaribu kufanya maskini mke wake apone. Na si . . . Alikuwa amesikia habari Zake. Akasema, "Ni nani huyo pale chini?"

Kasema, "Huyo ni yule nabii kutoka Galilaya."

164 Akasema moyoni mwake, hakuna Maandiko kwa hilo, "Ninamwamini. Na kama ninaweza tu kugusa upindo wa vazi la Mtu huyo mwenye haki, nitapona." Hmm! Kama aliweza kufanya hilo pasipo na ahadi ya Maandiko, tunapaswa kufanya nini na ahadi ya Maandiko? Alipenya akapita.

165 Huyo hapo mchungaji, wote hao, wakisimama hapo kumkosoa, wakimdhihaki Yeye na kujaribu kumfanya aondoke nchini. Hawakutaka watu wao wasumbuke mioyoni mwao. Wasingeweza kushirikiana katika mkutano. Hakuna kitu wangaliweza kufanya.

166 Bali Yeye alikuja kuwa na mkutano, kwa vyovyote. Mnaona? Na kwa hiyo alikuwa anaenda kuwa nao, kwa vyovyote. Kwa hiyo tunaona, kulikuwako na wawili au watatu pale wangemsaidia, kwa hiyo mlete ng'ambo ya mto, kwa vyovyote. Kwa hiyo basi tunaona, kwamba kwenye . . . wakati alipoanza kutembea akipanda juu.

167 Maskini mwanamke huyu, akasema, "Vema, Mtu kama huyo, muhimu sana, mimi sina maana Kwake."

168 Na wengi, baadhi yao wakaanza kusema, "Ah, nitambulishe Kwake, kwa sababu ni—ninataka kuona kama Yeye ni nabii au la." "Ah, basi, vema, nitambulishe, Simoni," *fulani-wa-fulani*. Kila mtu, "Aloo, Rabi! Mbona, wanasema Wewe ni nabii."

169 "Naam. Naam. Asante, bwana. Bwana akubariki." Endelea, namna hiyo, alipoendelea kusonga mbele.

170 Kitu cha kwanza, maskini mwanamke huyu aliendelea kujipenyeza kati ya wanaume hao, na kote, mpaka akaligusa vazi lake la nje sasa. Vazi la Kipalestina hupwaya; lina ninii la—vazi la ndani, pia, kuzuia vumbi kwenye mikono. Na Yeye asingehisi huo kimwili. Basi, akamgusa. Hilo hasa ndilo analotaka kufanya. Alitoka akarudi nyuma na kuketi.

171 Hiyo ilikuwa ndiyo saa yake yenye giza kuliko zote, fedha zote zilikwisha, kila kitu kingine, ndipo Yesu akaja. Yesu aligeuka akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Akaangalia huko nje, naye huyo hapo. Akasema, "Imani yako imekuokoa."

172 Maskini yule mwanamke kisimani kimaadili, asingeweza kuwa mbaya zaidi. Alikuwa na. . . Alikuwa tu ndio kwanza amchukue mume wake wa sita, kwa hiyo kimaadili asingeweza kuwa mbaya zaidi. Saa yake yenye giza kuliko zote, hapana shaka, kwenda pale juu na kusema, "Jinsi nilivyo mwovu! Mimi ni kijana mwanamke, mrembo, lakini ninaanza kuzeeka kidogo tu. Ninaingia katika miaka yangu ya ishirini sasa, kwa hiyo ninii yangu. . . haiwezi kwenda. . . "

173 Sasa kumbuka tu, dada, ukipita hiyo ishirini, wakati ukipita umri wa miaka ishirini na miwili, unadhoofika, haijalishi kama unafikiria hudhoofiki, au la. Unadhoofika. Naam. Unadhoofika. Kila mwanamume anadhoofika, pia. Wewe, unapofikia karibu. . . unaninii. . .

174 Hiyo ndiyo niliuliza kwenye mkutano wa Kiwanis wakati mmoja. Nikasema, "Niambieni jinsi ilivyo, kwamba, nikila chakula, kinatengeneza seli za damu nami ninakuwa mkubwa zaidi na mwenye nguvu zaidi. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula kitu kile kile ninachokula sasa. Nilizidi kuwa mkubwa na mwenye nguvu zaidi wakati wote. Sasa, tangu nilipopitisha miaka ishirini na miwili, haijalishi ninakula kiasi gani, jinsi nilivyojitunza vizuri, ninazidi kuwa mnyonge na mzee. Kwa nini, kama nikiyafanya upya maisha yangu sasa, je! itakuwa kwamba. . .? Kila wakati nikila, ninafanya upya maisha yangu, maana ninaingiza seli za damu. Kwa nini hakinijengi sasa kama kilivyofanya wakati huo?" Huwezi kuithibitisha kisayansi, kama ilikupasa kuthibitisha.

175 Ni miadi aliyofanya Mungu. Nawe utakutana nayo, pia. Likumbuke tu jambo hilo. Unaijia. Ukimimina maji kutoka kwenye jagi, ndani ya bilauri, ijae nusu, na kisha umimine upesi zaidi na yanapungua; niambie yanapoenda na kinachotendeka. Mnaona? Ni kwa sababu Mungu alifanya miadi.

176 Na maskini mwanamke huyu, alijua kwamba siku zake zilikuwa karibu zimekwisha basi. Kazi yake ingeharibika. Kwa hiyo alikuwa akifikiria kuhusu, "Nitafanya nini? Bali," akasema, "unajua, daima nimewazia kwamba siku moja huenda Masihi

akaja.” Alipanda juu kule, kisimani. Kwa kawaida ni wakati unapowaza juu Yake, ndipo Yeye huja. Mnaona? Na kwa hiyo akapanda kule juu; giza. Wanawake wote walikuwa wameenda. Naye alikuwa mwenye sifa mbaya, asingeweza kuzungumza nao, au chochote. Alikuwa na viopoleo, naye akashusha winchi. Ndipo akaanza . . .

Akasikia Mtu akisema, “Nenda kamwite mumeo kisha mje hapa.”

Akasema, “Mimi sina mume.”

177 Akasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule uneyeishi naye sasa si wako.”

178 Ndipo akaanza kudhikika. Akasema, “Bwana, naona kuwa Wewe ni nabii. Ninajua kwamba ajapo Masihi, hivyo ndivyo atakavyofanya.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

179 Loo, wanafunzi walikuwa baharini, usiku mmoja, na matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Labda umeketi hapa, usiku wa leo, katika njia ii hii, matumaini yote yamekwisha. Maskini mashua yao ilikuwa imejaa maji na kadhalika. Ndipo, Yesu, waliondoka bila Yeye.

180 Ndipo basi walipokuwa wakipiga makelele na kulia, na kushangaa ni nini kitakachotukia, ni kitu gani kilichofuata? Walimwona Yeye akija akitembea juu ya bahari. Unajua nini? Walimwogopa. Ilionekana kama pepo, ilionekana kana kwamba ni namna fulani ya mizuka au kitu kingine. Mnaona? Huyu hapa anakuja Mtu akitembea pale, kama kivuli juu ya maji, nao wakaanza kupiga makelele. Kitu cha pekee kilichoweza kuwasaidia, na hapo walikiogopa.

181 Ikiwa hiyo si hasa jinsi ilivyo leo, wanakiogopa, wanaogopa Hicho.

182 Lakini ni nini kilichotukia? Kwenye wakati tu wa woga wao, Sauti ikatokea, kasema, “Msiogope. Ni Mimi.” Ndipo, Yesu akaja. Loo, jamani! Yesu akaja. “Msiogope. Ni Mimi.”

183 Sasa, Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nashangaa, usiku wa leo . . . Inanibidi kuacha sehemu ya somo langu hapa. Bali nashangaa, usiku wa leo, ikiwa sisi, kwenye saa hii . . . Bwana amekuja kama alivyoahidi, Naye anawaita watoto Wake wanaoamini wapate kumtambua katika Neno Lake, akilidhihirisha. Nashangaa ikiwa Yesu ametujia. Hii ndiyo—hii ndiyo saa yenye giza kuliko zote kanisa liliyopata kuona.

184 Sasa, wajua nini? Kila kanisa, karibuni, itabidi liwe mshiriki wa hilo—hilo Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na wakati mkifanya hivyo, mtapoteza haki zenu za kiinjilisti mtakapofanya hivyo. Na msipofanya hivyo, basi hamwezi kuwa madhehebu tena. Maana, kila dhehebu sharti lijiunge na hilo. Mmesoma kuhusu hilo, kama vile tu mimi nimesoma. Ni saa yenye giza

kuliko zote ambayo kanisa hili dogo limewahi kuwa nayo. Kila kitu kimetoka kulikimbilia. Pentekoste, loo, jiamsheni!

185 Na moja kwa moja kwenye saa hii yenye giza kuliko zote, basi huyu hapa Yesu anakuja, kuthibitisha Yeye yu pamoja nanyi. Yeye yupo hapa, mnaona, saa yenye giza kuliko zote.

186 Nilisikia hadithi fupi, inahitaji tu dakika moja kuisimulia. Mwanamke ali—aliitwa, jimbo lilikuja kumtazama, maana alilemewa na umaskini. Alikuwa na mwana, naye alikuwa ameenda India wakati fulani uliopita. Na yeye, rafiki mwema sana, na mvulana mzuri. Na kwa hiyo mwanamke huyo akawa hivyo, bila chakula na kadhalika, mpaka ikabidi jimbo lije kuchunguza, kwa ajili ya chakula cha msaada wa jimbo kwa ajili yake. Ndipo walipokuwa hapo, mtu huyo akasema, "Vema, huna wapendwa wowote wa kukusaidia?"

Akasema, "Loo, ninaye mwana."

Kasema, "Hufanya kazi gani?"

Kasema, "Loo, yeye ni m—m—mhandisi umeme huko India."

"Vema, ameajiriwa na nani?"

Kasema, "Serikali ya Marekani."

"Mbona," kasema, "kwani hakusaidii?"

Kasema, "Vema," kasema, "ha—hanisaidii mimi. Lakini . . . "

187 Kasema, "Vema, basi ni kwa nini usimwombe badala ya kuliita jimbo?"

188 Akasema, "Yeye ni mvulana mzuri sana. Huniandikia barua za kupendeza sana." Ndipo kasema, "Mwajua, ninampenda, kwa hiyo siwezi kumwambia kwamba ni—nina ukosefu hivi."

189 Wakasema, "Yeye—yeye hukuandikia barua, na unasikia kutoka kwake, na kadhalika?"

"Ndiyo."

"Na bado hakusaidii?"

190 Kasema, "La." Kasema, "Lakini hunitumia baadhi ya picha za kupendeza kuliko zote nilizopata kuona maishani mwangu." Ndipo akasema . . .

Kwa hiyo mtu huyo akasema, "Hebu nione baadhi ya picha hizo."

191 Akasema, "Vema, bwana. Ninazo moja kwa moja hapa kwenye Biblia." Naye akazifungua, na kuanza kuzitoa. Unajua zilikuwa ni nini? Hawala za fedha kutoka India, zikiwa na picha. Zote zilikuwa na picha, unaona, hawala za fedha. Alikuwa na maelfu ya dola, ila tu hakujua thamani yake. Yote ilifichwa Bibliani.

192 Nashangaa, usiku wa leo, ikiwa Yesu hangeweza kutufunulia kinachofichwa katika Biblia hii, kwa ajili yetu. Tu matajiri katika neema Yake na Rehema Yake. Nashangaa iwapo

angeweza kuja na kutuita. Hebu tuangalie kote Bibliani na tuone tulicho nacho ndani Yake, huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa kitambo.

193 Baba wa Mbinguni, hebu rehema Yako . . . Upo hapa, Baba. Mbona, ninatambua tu hilo. Mbona, Wewe ulisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nami nipo papo hapo katikati yao." Sasa, hilo, "Mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita kamwe." Tusaidie, usiku wa leo, sasa, tunapowaombea watu hawa wagonjwa, kwa dakika chache zijazo. Jitambulishe Mwenyewe, Bwana. Yesu, njoo na ukawaite wagonjwa, (Utakuja?) ili waweze kujua kwamba Wewe ni—Wewe ni Mungu aliyepo kila mahali. Upo hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kupitia Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

194 Marafiki, dakika moja tu ama mbili hadi itakapokuwa wakati hasa wa kufumukana, bali hebu na tuitishe mstari mdogo wa maombi. Hivi mngependa kuwa nao? Inua mkono wako, kama uko—uko tayari kukaa dakika zingine kumi, kumi na tano. Vema. Mungu awabariki. Ninii tu—ninii tu . . . Je! ni sawa na msimamizi hapo, sawa kwetu kuchukua hizo? Asante, sana.

195 Sasa, Billy yu wapi? Ulisambaza kadi ngapi? A, B, C. Ni zipi tulisambaza kwanza, za A? Je! tulimaliza kuita za A, usiku wa kwanza hapa? [Mtu fulani akasema, "Naam."—Mh.] Hebu tuite kuanzia A tena. Hebu tuone, tulianzia wapi, Billy? Unakumbuka? Moja, sivyo? Naam. ["Moja."] Moja mpaka yapata . . . Hebu tuite kuanzia mahali pengine. Hebu tuone, tutaita kuanzia wapi? Hebu tuseme sabini na tano.

196 Ni nani aliye na kadi ya maombi A sabini na tano? Inua mkono wako. Basi hilo ni jema, sawa. Tumeipata. Njoo moja kwa moja hapa chini, basi, sabini na tano.

197 Sabini na sita, inua mkono wako. Sabini na sita, upesi sana. Vema. Nani? Huwezi kusimama? Au, la, iko huko nyuma kabisa. Samahani. Sabini na sita.

198 Sabini na saba, sabini na saba, waweza kuinua mkono wako. Yeyote aliye na kadi ya maombi . . . Loo, mtu fulani hapa. Vema. Papa hapa, bwana, sabini na saba.

199 Sabini na nane. Upesi sasa, inua mkono wako, sabini na nane. Sabini na nane.

200 Sabini na tisa, themanini, themanini na moja, na mbili, na tatu, na nne, na tano. Hebu hiyo . . . Simama tu hapo, upesi sana. Kuwa tu na ninii . . .

201 Sasa, ninyi wengine mtaweza kuketi tu kimya kabisa, kwa kicho? Msisogeesogee sasa. Hebu hao, walioitwa pekee.

202 Sabini na tisa, themanini. Themanini hadi themanini na tano. Inaonekana kana kwamba wao si . . . Labda baadhi yazo ni kadi zilizosambazwa usiku wa siku nne au tano zilizopita. Huenda ikawa sasa . . . Themanini na tano hadi tisini, njoni hapa,

njoni huku juu kutoka hapo. Katika za A sasa, A, kadi ya maombi A, kuanzia sabini na tano, themanini, themanini na tano, tisini. Hiyo itakuwa watu kumi na watano. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi . . . Hao hapo. Sawa. Hilo ni jema. Hilo litakuwa sawa, kwa dakika moja tu sasa.

203 Sasa ni wangapi, ninyi wengine huko nje, wanao... wanaoamini kwamba—kwamba mnaweza kufanya kama maskini mwanamke yule alivyofanya, kugusa upindo wa vazi Lake? Inua mkono wako, useme, “Ni—ni—ni—ninaamini. Kweli ninaamini ninaweza kugusa upindo wa vazi Lake.”

204 Sasa Bwana ashakuja. Sasa ataninii . . . Yuko tayari kukuita, ikiwa tu utamwamini. Sasa usiwe na shaka juu Yake. Mwamini. Kuwa na imani sasa. Kuwa na kicho sana. Amini kwa moyo wako wote sasa ya kwamba Bwana amekuja na anakuita.

205 Sasa, wakati mstari wa maombi unapopangwa hapo chini, nadhani baadhi ya ndugu wanasaidia kupanga mstari wa maombi juu kwenye—jinsi walivyo kwa namba zao. Sasa kila mtu ana kadi. Ni . . . Ni kadi ngapi zaidi zilizomo humu ndani? Hebu tuone mikono yenu. Zishikeni. Tutaombea kila mmoja wao. Sijali ni akina nani, tutaninii . . . Bwana akinijalia kuishi, nitaombea kila mmoja kabla niondoke Jumapili.

206 Sasa kumbukeni, kuna kiamshakinywa cha wahudumu asubuhi. Na je! mmekitangaza, mahali kilipo? Kimetangazwa. Vema. Ambacho, kama unaweza, njoo. Ingekuwa . . . Nadhani ninapaswa kuhubiri, mapema asubuhi pale? [Mtu fulani anasema, “Naam, kiamshakinywa.”—Mh.] Vema. Sawa. Safi. Vema.

207 Nini, wasemaje, “Sikukusikia”? Niliita karibu, nafikiri, kumi na watano. Sabini na tano, themanini, themanini na tano, tisini, kitu kama hicho. Hiyo . . . Hiyo itakuwa sawa. Kama tu . . . Vema. Anzeni kuwatuma huko. Kama unaangalia, sasa hiyo ni . . . Mnaona?

208 Sasa, kila mtu awe na kicho kabisa. Sasa, sasa sikilizeni. Ninajua inawabidi kwenda kazini asubuhi. Kazi yako ni muhimu. Ninajua hiyo. Watoto wako wanakungojea. Mayaya; alisema ataondoka saa tatu na nusu. Bali hebu tusubiri tu. Ni nini kilicho muhimu zaidi, kujua kama hili ni Kweli au la? Ni nini kilicho muhimu kuliko nafsi yako? Sasa, kama Biblia hii imeahidi hili, Mungu hulitimiza, hilo ndilo jambo muhimu kuliko yote niwezayo kuwazia. Mnaona?

Kuna kiti kule, pamoja na vipaza sauti, na hivyo ndivyo vilivyokuwa vikipiga kelele.

209 Sasa angalia. Sasa, kumbukeni, hebu kila mtu atulie kabisa sasa. Natumai sijawashawishi sana kuwafanya mfikirie kuwa mimi ni namna fulani ya madhehebu au kitu kama hicho, kwamba ningekuwa yule Mtu, Bwana Yesu. Hamwamini hivyo, sivyo? Hakika hamwamini. Mimi ni mtumishi wake. Mimi ni

mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Bali, katika hili, wakati umewadia ambapo Yeye ametoa karama.

210 Nilifanyiwa uchunguzi hivi majuzi tu, wakati kundi la madaktari wa tiba waliponiweka chini ya uchunguzi wa makini, kunipima, kupimwa kiwimbi. Na unajua kile walichotoka na kuniambia?

211 Kasema, "Sijapata kuona kama hili maishani mwangu." Akasema, "Unajua, wewe ni. . ." Kasema, "Mtu, kwamba wakati hisi zako tano ambazo wewe. . .mwili unadhibitiwa kwazo." Kasema, "Sasa, sasa, ninii yako. . ." Kasema, "Hiyo ni yako ya kwanza, dhamiri. Unaishi humo. Lakini wakati hisi zako tano zinapokuwa ha—hazifanyi kazi, basi una dhamiri ya ndani. Hiyo iko mbali na wewe. Lazima uwe umekufa kwa hisia hizi au chochote hapa, wakati ukirudi nyuma kwenye dhamiri hii ya ndani na unaota." Kasema, "Kuna sehemu yako fulani ambayo huenda mahali fulani. Ndipo wewe, wakati ukiamka, kurudi kwa hisi zako tena, unatikiswa kurudishwa hapa, unakumbuka kile ulichoota."

212 Ni wangapi wamewahi kuwa na ndoto? Hakika, miaka iliyopita, ninyi nyote. Vema, kuna sehemu yako fulani mahali fulani, maana bado unaikumbuka moyoni mwako. Hiyo ni kweli? Basi hiyo ilikuwa ni dhamiri yako ya ndani.

213 Akasema, "Hiyo ndiyo ya kawaida. Bali," kasema, "Kasisi Branham," kasema, "makumi elfu mara maelfu ya watu tunaowachunguza, hatujampata mtu kama wewe."

Nikasema, "Je! nina wazimu?"

214 Akasema, "Sidhani watu huja kote ulimwenguni, kuzungumza na mwendawazimu."

Nami nikasema, "Vema, je! nina wazimu? Ninajua nina wasiwasi."

215 Akasema, "Si zaidi ya vile mhudumu yeyote au daktari, yeyote anayehusika na umma."

Nikasema, "Ni nini kisicho cha kawaida sana?"

216 Akasema, "Unajua nini? Dhamiri zako mbili zinakaa moja kwa moja pamoja." Kasema, "Ungeweza kuota ndoto huku macho yako yote mawili yamefumbuka." Mnaona?

Hakujua alikuwa ni kitu gani, nini kuhusu hilo. Nikasema, "Je! hiyo ni kweli?"

217 Akasema, "Naam. Haitakulazimu kwenda usingizini kuota ndoto."

218 Nikasema, "Daktari, uliwahi kusoma kwenye ninii. . . kuhusu ono? Unajua ono ni kitu gani?"

Akasema, "Je! huo ni msamiati wa Biblia, Bw. Branham?"

Nikasema, "Naam."

219 Akasema, "Vema, sijui chochote kuhusu Biblia." Akasema, "Nisingeweza kujua unachokizungumzia."

Nikasema, "Je! uliwahi kusoma Biblia?"

Akasema, "Naam."

"Rudi usome katika Biblia kuhusu manabii wa kale wa la Kale."

"Loo," akasema, "hilo! Kitu gani? Ati waliona mambo kimbele?"

"Naam." Nikasema, "Hilo hunitokea, bwana."

220 Akasema, "Hilo, nina furaha wewe . . . Hilo latosha. Vema, jambo ndilo hilo, unaona." Akasema, "Unajua nini? Unapaswa—unapaswa kuingia na kuturuhusu tuchunguze hili." Kasema, "Hili litakuwa uchunguzi mkuu wa kisayansi."

Nikasema, "Ngoja kidogo, daktari. Je! umewahi kuwa na ndoto?"

Akasema, "Naam."

221 Nikasema, "Basi niotee ndoto. Niambie kitakachotukia kesho. Usingeweza kufanya hivyo hata ufanye nini. Unaona? Yule aliyekupa ndoto hiyo hana budi kufanya hivyo."

222 "Wala siwezi kuona ono. Lazima iwe ni Yeye anayeruhusu maono. Siwezi kuyaona mpaka aniambie. Sijui la kusema mpaka aniambie niseme. Bali ni karama, unaona, ambayo nilizaliwa na hiyo. Jambo la kwanza ninalokumbuka maishani mwangu lilikuwa ni kuona ono. Na halijawahi kukosea hata wakati mmoja." Mnaona? Ni ninii yako—ninii yako . . . Hiyo ndiyo sababu unawaona watu . . .

223 Tunao uigaji mwingi. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini siku zote tutakuwa na huo. Hakika.

224 Nilisoma hadithi ya Martin Luther, kwenu Walutheri. Hadithi ya Martin Luther ilisema, "Halikuwa jambo la kigeni sana kwamba Martin Luther angeweza kulipinga kanisa Katoliki na kuponyoka na hilo; lakini angeweza kuinua kichwa chake dhidi ya ulokole wote uliofuata uamsho wake, na bado abaki sawa na Maandiko." Jambo ndilo hilo. Naam.

225 Hilo halina uhusiano wowote nao. Unawajibika mbele za Mungu . . . Kwa sababu, unaona, ni karama tu. Mnaona? Unajishusha hapa, na kisha Bwana ananena.

226 Sasa, hapa. Hapa, je! huyu ndiye mwanamke huyo? Sasa, hapa, hili linapaswa kulithibitisha, sasa, iwapo kila mtu atakuwa na kicho kabisa, kwa dakika chache tu. Labda mgeni yupo hapa. Sasa huyu hapa m—msichana, si—sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ni mgeni kwangu. Simjui.

227 Bali hapa tunakutana, kama tu vile Yohana Mtakatifu 11 . . . Nimekuwa huko, usiku wa leo, unaona, wakati . . . Yohana Mtakatifu 4, namaanisha, ambapo Yesu alikutana na mwanamke

kisimani. Nilikuwa nikinena habari zake. Labda mwanamke huyo alikuwa na umri mdogo kuliko Yeye. Na Yeye akamwambia mahali shida yake ilipokuwa. Na kwa hilo, akasema, "Sasa, Bwana, Wewe, naona kuwa Wewe ni nabii."

228 Sasa, unaona, nabii ni yule aliyejiliwa na Neno la Mungu. Unabii wa siku hiyo, Neno linalopaswa kutimizwa katika siku hiyo, humjia mtu huyo, na Yeye ndiye hilo Neno lililo hai kwa ajili ya siku hiyo.

229 Akasema, "Naona kuwa Wewe ni nabii. Sasa tunamngojea yule nabii." Kama utafuatilia marejeo hayo huko nyuma, yanakurejesha moja kwa moja kwa—kwa nabii huyo. Kasema, "Tunajua ajapo Masihi, hayo ndiyo atakayotenda. Atatuambia mambo hayo."

Akasema, "Mimi Ndiye, ninayezungumza nawe."

230 Ndipo akaenda na kusema "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Je! huyu siye Masihi?" Na watu wote wakaliamini.

231 Sasa, Yeye aliahidi kwamba, "Kazi alizozifanya Yeye, waaminio wangezifanya pia." Na sasa, katika siku hizi za mwisho, amethibitisha Kuja Kwake kulikokaribia kwa hilo, wakati anapojifunua Mwenyewe kwa njia ile ile kama alivyofanya Sodoma.

232 Je! umekuwa ukisikiliza Jumbe juma hili? Unaamini huo kuwa ni Kweli? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sasa, tukiwa hatufahamiani mmoja na mwenzake, hiyo ni kweli, sivyo? ["Ndiyo."] Ili tu kwamba watu waone, inua mkono wako, ili watu waone.

233 Sijawahi kumwona mwanamke huyu, maishani mwangu. Sijui chochote kumhusu hata kidogo. Mnaona? Yeye ni mwanamke kijana tu, mwenye umri mdogo sana kuliko mimi. Tumeachana kwa miaka mingi kwa kuzaliwa, umbali wa maili nyingi, nasi hapa tunakutana, mara ya kwanza. Hapa sote wawili tunasimama hapa, watu wamezunguka kote, taa, kila kitu kingine. Tumesimama hapa katika Uwepo wa Mungu. Nami ninazungumza nawe, kujua, kwanza, kama upako huo utakuja juu yangu. Na kama ukija, basi nitaweza kufanya hivyo. Bila Huo, siwezi. Sasa, jambo pekee nifanyalo ni kuomba tu na kuweka mikono juu yako, kama vile mchungaji wako angefanya, ama yeyote yule, na kuendelea. Unaona? Ni karama. Mimi, kama nijuavyo, nimejiachilia kwa Huo. Bali, hata hivyo, siwezi kuufanya uje. Lazima Yeye aje. Hauna budi kuja, Wenyewe.

234 Sasa iweni tu na kicho. Upo hapa. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninamweka kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa kaeni kimya. Lolote likitendeka, nitaweza kulidhibiti, ikiwa hamtaruka tu na kuanza kufanya yasiyofaa. Kaeni kimya. Kifafa na vitu vingine wakati mwingine huingia kwenye mkutano na kunyakua tu dazeni ya

hao, namna hiyo. Ni wangapi wameona kama hilo likitendeka katika mkutano wangu? Hakika. Mnaona? Hakika. Lakini ninyi kaeni tu kimya. Ninawajibika kwa hilo. Lakini mkiwa na kiburi, siwajibiki, maana ni adhabu.

235 Sasa, mwenyewe sijui kilichomleta mwanamke huyu hapa. Sasa, yeye anajua hilo sasa, wakati huu, kwamba jambo fulani linaendelea. Unaona? Maana, moja kwa moja kati yangu na yeye, anaanza tu kutoweka. Ni ile Nuru ikija.

236 Sasa, mwanamke huyo kwa kweli, jambo lake kuu lililomleta hapa, anasimama kwa ajili ya mtu mwingine. Anaye mtu ambaye ananinii—anamwombea. Na huyo ni m—m—m—mtu aliye katika hali mbaya sana, katika ugonjwa wa akili. Ni dada. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, inua mikono yako. Ana ugonjwa wa akili. Sasa angalia.

237 Kwa hiyo watu wanasema, "Nafikiri alibahatisha tu hiyo." La, la. Mnaona? Kamwe sikubahatisha hiyo.

238 Sasa tazama. Ni mtu mwema sana, roho nzuri. Sasa hebu kidogo tu. Sasa niangalie mimi. Na hilo ndilo Petro na Yohana walilosema, kwenye lango, "Sasa niangalie mimi." Unaona? Ilionekana kuwa kuna kitu kingine moyoni mwako. Naam. Unaumwa, mwenyewe, na namna fulani ya kupatwa na kizunguzungu, kama unavyopata. Una hiyo. Hiyo ni kweli.

239 Unacho kitu kingine moyoni mwako, unachotaka kujua habari zake, na hicho ni kwa ajili ya yule ndugu. Yuko hospitalini hapa. [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unataka nikuambie jinsi alivyofikia kuwa kule? Alikuwa kwenye ajali ya motokaa. Hiyo ni kweli. A-ha! Je! unaamini unapokea kile ulichoomba? Basi nenda zako. Yote yamekwisha, basi. Unaona?

"Ikiwa unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

240 U hali gani, mama? Sasa, je! unaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, yeye yule jana, leo, na hata milele? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Ikiwa atanifunulia kilicho shida yako, unaamini kwamba Yeye anaweza kufanya hivyo? ["Hakika ninaamini."] Vema. Sasa naomba ajalie hilo.

241 Kitu kimoja kinachokusumbua, naam, a-ha, kwanza, umefanyiwa upasuaji fulani. Na umeondolewa titi, limekatwa. Halafu, umeumiza titi lako, titi lako lingine, na hiyo ndiyo shida yako. Hutoki hapa. [Dada huyo anasema, "La."—Mh.] Unatoka karibu na mto wa ninii. . . Unatoka Louisville, Kentucky. ["Na karibu na wewe."] Nalo jina lako ni Bibi Lumpkins. Mungu akubariki. Hiyo, hiyo ni kweli. Umekuwa maskanini. Sikukutambua. Bali hiyo ni kweli kabisa. Enda zako, ukiamini sasa. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Vema.

242 Njoo sasa. Je! unaamini kwa moyo wako wote, bwana? Unaniamini kuwa ni mtumishi Wake? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Je! unaamini kwamba—kwamba wewe,

unapokuja, unakuja tu kama Simon Petro alivyokuja wakati ule? Unaona? Hunijii mimi. Unamjia Yeye. Nami ni mwakilishi wake tu. Unaona? Yeye . . . mimi . . . Sisi ni ma—ma—matawi; Yeye ni mzabibu. Sasa, kama Bwana Yesu . . . Tukiwa hatufahamiani kabisa mmoja na mwenzake, nadhani hatufahamiani. Na kama—na kama hatufahamiani kabisa, na Bwana Yesu anaweza kunifunulia jambo kama alivyomfunulia Simon Petro, baadhi ya hao wengine, walipokuja, litakufanya uamini, kwa moyo wako wote? Utaamini? ["Naam."] Sasa, vema, bwana. Sasa wewe niangalie kwa dakika moja.

243 Sasa, shida yako, ninakuona. Ni kitu kuhusu tumbo. Iko katika . . . Ni uvimbe kwenye tumbo. [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hiyo ni kweli, uvimbe tumboni mwako. Tuseme, jambo jingine, wewe ni mhudumu, pia. ["Naam."] Naam, bwana. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Unaamini Mungu anakujua? ["Ninaamini, kwa moyo wangu wote."] Yote, kwa moyo wako wote. Vema. Kasisi Brown, nenda, uwe mzima, Yesu Kristo . . .

244 Amini. Unaamini Mungu anaweza kuponya yabisi kavu yako na kukufanya mzima? Nenda, ukiliamini basi. Useme, "Asante, Bwana Yesu."

245 Njoo, mama. Unasumbuliwa na ugonjwa wa neva. Unaamini kwamba Mungu anaweza kukuponya huo? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Vema. Nenda tu, ukisema, "Bwana asifiwe!" Unaona, gurudumu dogo likigeuka *hapa* chini. Lilikuwa likigeuka *hapa* juu. Ulikuwa mtu mdogo mwenye furaha ulipokuwa ungali mchanga, umejaa furaha na mchangamfu. Na ghafla, jambo fulani likatukia. Sasa nenda tu pale juu, na uamini hilo tena. Anza tu, ukiwa na furaha, ukishangilia, Yesu Kristo atakuleta kwake. Mungu akubariki. Nenda, amini sasa, kwa moyo wako wote. Vema.

246 Unaamini? Unalemaa, pia. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuuponya na kukufanya mzima? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema. Nenda tu, useme, "Asante, Bwana Yesu," na kwa moyo wako wote.

247 Unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya hiyo pumu na kukufanya mzima, mwanangu? Nenda zako, ukishangilia, ukiwa mwenye afya na mwenye furaha. Pia, udhaifu, tezi kibofu, na yabisi kavu. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya huo, akuponye? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Ukiamini kwa moyo wako wote, nenda zako, ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana."

248 Hebu kidogo tu sasa. Hebu dakika moja. Jambo fulani lilitukia. Mtu tofauti na huyu. Amini tu sasa, kwa moyo wako wote.

249 Ni mama huyu anayeketi moja kwa moja *hapa*, akiugua shida ya mgongo. Unaamini kwamba Yesu Kristo anakuponya,

kwa moyo wako wote? Vema. Unaweza kupata ulichoomba, basi. Unaona? Bwana Yesu akuponye na akupe afya.

250 "Ikiwa unaweza kuamini hilo, mambo yote yanawezekana kwao waaminio." Unaamini hilo kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unafikiri nini kuhusu hilo, ukiwa umeketi hapo, ukiugua hiyo ngiri? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya hiyo ngiri na kukupa afya? Naam. Unaamini atakuponya? Vema. Unaweza kupata ulichoomba. Bwana akubariki.

251 Mnaona, Yeye yuko huko nje sawa tu na alivyo hapa. Hiyo inapaswa tu kuturarua vipandevipande, sivyo? Unafikiri Mungu ataponya hicho kisukari na kukufanya kuwa mzima, na uende nyumbani, hali ya damu itakuwa . . . Nenda Kalvari, kwa ajili ya kuongezwa damu, itakwisha kabisa. Nenda, amini kwa moyo wako wote. Usitie shaka. Amini tu, kwa moyo wako wote, kwamba Mungu atakuponya.

252 Njoo hapa. Unao ugonjwa ulio hatari kuliko yote yaliyomo duniani. Huo ni ugonjwa wa moyo. Bali Yesu huishi moyoni. Je! unaamini kwamba atakuponya katika moyo huo? Vema. Nenda zako, ukisema, "Asante, Bwana Yesu," na akufanye mzima.

253 Nenda, ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo alikuponya kutokana na ugonjwa huo wa tumbo, anakufanya mzima. Vema.

254 Unaamini? Unaamini, nisiposema neno, nikuwekee tu mikono, utapona, kwa vyovyote vile? Bwana akubariki. Amini tu kwa moyo wako wote.

255 Unaamini, nikiweka mikono juu yako, utapona, pia? Njoo. Katika Jina la Yesu Kristo, na aponywe.

256 Njoo. Sasa, unajua ninajua shida yako. Lakini, hapo, hata nisipokwambia, unaamini haitakubidi kutolewa hicho kivimbe, na kitakuwa tu sawa tangu sasa? [Dada huyo anasema, "Hakitaondolewa."—Mh.] Vema. Vema. Endelea tu basi, mwamini Mungu, utapata afya na kuwa mzima. ["Unafikiri nina kasoro fulani?"] Uki—ukiamini tu hilo, Yeye atakiondoa. Hata haitakubidi kuwa nacho, ukiamini tu kwa moyo wako wote. ["Haitabidi kiondolewe."] Bwana asifiwe.

257 Sasa je! unaamini kwamba Mungu huponya kansa, na kuwafanya watu, walio na kansa, kuwa wazima? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Vema, bwana. Nenda zako, na useme, "Asante, Bwana, nitakuwa mzima." Nawe utakuwa sawa.

Sasa Yesu amekuja na anakuita. Unaamini hilo?

258 Unaamini hilo, unayeketi hapo, mama, mnene kiasi, ukiwa na ugonjwa huo wa mapindi? Unaamini Mungu atakufanya Mzima? Vema. Mnaona? Ukiangalia hapa tu, endelea tu kuangalia moja kwa moja, na kuamini. Na huo . . .

259 Mama huyo anayeketi hapo, aliyetikisa kichwa chake, moja kwa moja kando yako. Hakujua cha kuwazia kuhusu hilo. Kama utaamini, yabisi kavu yako itaondoka, pia. Vema.

Unaamini kwa moyo wako wote?

260 Mwanamume huyu mzee anayeketi hapa, kutoka Okeechobee, huko, unaamini kwamba Yesu Kristo atayaponya macho yako yanayopofuka? Unaweza kupata unachoomba, kama utaomba.

261 Bwana amekuja na anakuita. Je! unamwamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi simama tu kwa miguu yako na umkubali, na useme, "ninakuamini, Bwana Yesu, sasa hivi. Nainua mikono yangu, nami ninaamini kwamba Wewe unaniponya sasa."

Bwana Yesu, wasikilizaji hawa ni Wako. Tumechelewa, Bwana.

> Lakini usinipite, Ee Mwokozi mpole,
> Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
> Unapowazuru wengine,
> Usinipite.
>
> Wewe ndiye Chemichemi ya faraja yangu yote,
> Zaidi ya uhai kwangu;
> Ni nani niliye naye duniani kando Yako?
> Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

Fanny Crosby kipofu alitoa tamshi hilo.

262 Bwana Yesu, usimpite yeyote wa hao, bali umpe kila mmoja wao uponyaji wao, usiku wa leo. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

263 Inueni mikono yenu sasa na muimbe sifa hizo. Nitawaombea. Vema. Kila mtu, mnamwamini?

264 Sasa, Bw. mpiga-kinanda, *Nitamsifu. Nitamsifu.* Tupe sauti. Vema.

Kila mtu, huku mmeinua mikono yenu sasa.

> Nitamsifu, nitamsifu,
> Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
> ya wenye dhambi;
> Mpeni utukufu, enyi watu wote,
> Kwani damu Yake imeondolea mbali kila waa.

265 Sasa peana mikono na mtu fulani karibu nawe, useme, "Mungu akubariki, rafiki. Ni—nina furaha kujua kwamba umemkubali Yesu kama mponyaji wako." Sasa, hiyo ni nzuri. Hiyo ni kweli. Peana mikono na useme, "Bwana ashukuriwe."

266 Sasa hebu tumwinulie mikono yetu, na tuimbe tena kwa yote ya mioyo yote; vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefumbwa, kwa mioyo yetu yote sasa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu, enyi watu wote,
Kwani damu Yake imeondolea mbali kila . . .

267 Hivi ametambulishwa miongoni mwenu vya kutosha hata mnaweza kumkubali? Je! mnaamini Yeye yupo hapa? Mnaamini kwamba huyo ni Yeye? Marafiki, kama ningeweza kushuka huko kwenye wasikilizaji na kumponya yeyote wenu, hakika ningefanya hivyo. Ningefanya hivyo kwa furaha. Ningefanya hivyo, kwa moyo wangu wote. Bali si—siwezi kufanya hivyo. Si—sina njia yo—yoyote ya kufanya hivyo. Lakini kitu cha pekee nilicho nacho, ni karama hii ndogo niliyokuwa nikiwaonyesha, na hiyo inatambulisha ahadi ya Maandiko kwamba Yesu Kristo yupo papa hapa pamoja nasi, akitimiza ahadi Yake. Loo, hilo lapaswa kuipasha moto mioyo yetu. Jamani, wazia tu kuhusu Yesu, hilo Jina la ajabu!

268 Wakati, ambapo Jina hilo lilitamkwa kwa mara ya kwanza, wakati Mariamu alipopanda akaja katika Uyahudi. Naye Elisabeti alikuwa ameshika mimba, naye maskini Yohana alikuwa na miezi sita, ndani ya tumbo la uzazi la mama yake, na hakuwa amesogea bado. Sasa, yeyote anajua, yapata miezi mitatu, au minne, ikiwa mingi sana, mtoto anacheza. Naye Elisabeti alikuwa si kawaida, yeye . . . Hakuwa amecheza. Alikuwa amejificha. Ndipo alipomwona Mariamu akija, uso wake mdogo uling'aa, kabisa na utukufu wa Mungu. Ndipo akasema, "Unajua . . . " Naye aliona kuwa alikuwa na mimba, ndipo akasema, "Nadhani wewe na Yusufu mshafunga ndoa?"

"La. Hatujafunga ndoa."

"Vema, a-ha, nawe una mimba?"

269 "Ndiyo. Roho Mtakatifu alinitia uvuli, na Yeye alisema Kitu hicho kitakachozaliwa ndani yangu kitaitwa 'Mwana wa Mungu.' Na nitaliita Jina Lake 'Yesu.'"

270 Na mara tu aliposema, "Yesu," mara ya kwanza ambapo Jina la Yesu Kristo lilipata kutamkwa kupitia mdomo wa mwanadamu, maskini mtoto mchanga aliyekufa ndani ya tumbo la uzazi la mama yake alimpokea Roho Mtakatifu na akaanza kuruka kwa furaha, ndani ya tumbo la uzazi la mama.

271 Jina la Yesu linapaswa kufanya nini kwa Kanisa lililozaliwa mara ya pili? Silipati. Utukufu kwa Mungu! Yeye ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Mpaji-uhai. Amina. Hebu na tumsifu. Inueni tu mikono yenu. Nami nitamsifu. Haleluya!

Ndipo Yesu Akaja Na Kuita SWA64-0417
(Then Jesus Came And Called)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 17 Aprili, 1964, katika Jumba la Mikutano la McKay huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org